# Nipashe

Ijumaa Novemba 3, 2023 • Tanzania 1000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581483

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




UKURASA 3

**WALIMU** wanaojitolea kutambuliwa rasmi

**WATUMISHI** 14 Wachunguzwa tuhuma za wizi wa milioni 60/-

UKURASA 5



**WCF** yaorodhesha majanga inayofidia madhila mfanyakazi

UKURASA 4



# Ufisadi Mfuko wa Kuzikana Polisi

**MAMILIONI** yaingizwa akaunti binafsi, hakuna vikao vya wanachama, ripoti ya uchunguzi yaanika majina... *Endelea Uk, 2*



Japhet Hasunga



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais wa Rwanda, Paul Kagame baada ya Mkutano wa Kimataifa wa 23 wa Baraza la Utalii Duniani (WTTC), jijini Kigali nchini Rwanda jana. **PICHA: IKULU**

## Mwinyi: Hospitali za Wilaya SMZ kuwapa chakula wagonjwa

UKURASA 3

RIPOTI MAALUM

## Shule yenye vyoo vilivyotitia, wanafunzi 950 hatarini kiafya

**Miaka mitatu watumia mbadala vichakani**

UKURASA 10



**MAFURIKO...** Vyombo vya moto vikipita kwa tabu kwenye mafuriko ya maji katika eneo la Jangwani, baada ya mvua kubwa kunyesha jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Ummy: Leseni udereva, usajili laini havitafunganishwa Bima ya Afya

UKURASA 2


**MICHEZO** **GAMONDI: NINA DAWA YA SIMBA** UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Mtaro ukiwa umeziba na kufanya maji yatuame kando ya Barabara ya Bagamoyo, eneo la Mwenge, baada ya mvua kubwa kunyesha Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Waziri Ummy: Leseni udereva, usajili laini havitafunganishwa Bima ya Afya

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu amesema kuwa kutokana na maoni na ushauri wa wadau mbalimbali na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya Ukimwi, serikali imeamua kutofungamanisha huduma za kijamii na Bima ya Afya.

Ummy alibainisha hayo bungeni juzi alipowasilisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Na. 8 wa Mwaka 2022.

Alisema kuwa kutokana na ushauri huo wa wadau, wameamua kukifuta kifungu cha 32 kilichokuwa kimefungamanisha huduma mbalimbali za kijamii na bima ya afya.

Alizitaja huduma zilizokuwa zimefungamanishwa ni pamoja na leseni ya udereva, bima za vyombo vya moto, viza ya kuingilia nchini, utambulisho wa mlipakodi, usajili wa laini za simu, hati ya kusafiria, uandikishaji wa wanafunzi kidato cha tano na cha sita na utoaji wa kitambulisho cha taifa.

Katika toleo letu la jana, iliripotiwa kimakosa kwamba huduma hizo zimefungamanishwa na Bima ya Afya. Tunaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza.

**Mhariri**

# Ufisadi Mfuko wa Kuzikana Polisi

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeanika ufisadi katika Mfuko wa Kufa na Kuzikana wa Jeshi la Polisi.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Japhet Hasunga akiwasilisha bungeni jana taarifa yao kuhusu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa hesabu zilizokaguliwa za serikali kuu na mashirika ya umma, alisema mfuko huo ulianzishwa na Inspekta Jenerali wa Polisi kupitia Kifungu Na. 7(2) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi, Sura ya 332.

Alisema kifungu Na. 66(1) na (2) cha sheria hiyo kimeainisha chanzo cha mapato ya mfuko huo kuwa ni michango ya askari ya Sh. 5,000 kila mwezi inayokatwa kutoka kwenye mishahara yao na kukusanywa kupitia akaunti Na. 20166004444 iliyoko Benki ya NMB.

Hasunga ambaye kitaaluma ni mhasibu, alisema ukaguzi huo ulifanyika kufuatia ombi la Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia barua yenye Kumb. Na. CJA.95/199/01/52 na Na. CJA.95/199/01/53 za Novemba 18, 2021.

**KILICHOBAINIKA**

Kiongozi huyo wa PAC alisema kuwa baada ya kufanya ukaguzi huo, kamati ilibaini ukiukwaji wa mwongozo wa mfuko na viongozi kujinufaisha.

Alisema ukaguzi maalum umebaini waliokuwa Meneja wa Mfuko huo, ASP Yusta Andrew Mwasanyamba (Julai 2018 hadi Januari 2020) na Insp. Abdallah Kambini (Februari 2020 hadi Novemba 2021) hawakuitisha vikao vya sekretarieti wala vya wanachama wa mfuko kinyume cha Kipengele 18.1 cha Mwongozo wa Mfuko.

Hasunga alisema kuwa katika kipindi cha uongozi wao, sekretarieti ya mfuko huo haikuwa imeundwa. Hesabu za mfuko hazikuandaliwa.

Alisema IJP Simon Sirro aliyekuwa mlezi wa mfuko kuanzia mwaka 2017 hadi 2022, alishindwa kumwelekeza Mwenyekiti kuitisha mkutano mkuu wa mfuko katika kipindi chote cha miaka mitano kinyume cha Kipengele Na.18.1 cha mwongozo wa mfuko huo.

Hasunga pia alisema Mwenyekiti CP Benedict Wakulyamba ambaye alikuwa Kamishna wa Utawala na Mwenyekiti wa mfuko huo alishindwa kutimiza majukumu yake.

Mwenyekiti wa Mfuko na IJP mstaafu Simon Sirro aliyekuwa mlezi wa mfuko walieleza kuwa aliyekuwa Meneja wa Mfuko, Insp. Abdalla Kambini aliyetoroka, alihusika na upotevu wa fedha na nyaraka za mfuko huo.

Alisema timu ya ukaguzi ilihakiki akaunti binafsi ya Abdallah Kambini Na. 20108003207 iliyoko Benki ya NMB (iliyokuwa ikipokea mishahara) na kubaini kupokewa Sh. milioni tano (miamala mitano ya Sh. 1,000,000) kutoka akaunti Na. 20106600444 ya mfuko huo kati ya Agosti 27, 2018 na Septemba 20, 2019.

Hasunga alisema kuwa kupitia ukaguzi, ilibainika wakati wa uhakiki kuwa miamala ya Sh. milioni 754.654 iliyolipwa kwa watiasaini haikuwa na nyaraka za malipo kwa wanufaika wala nyaraka za matumizi ya fedha hizo.

Alisema kufuatia kukosekana nyaraka, timu ya ukaguzi kupitia barua yenye Kumb. Na.CTA.35/364/01D/107 ya Februari 28, 2022 ilimwomba IGP kuwezesha upatikanaji watiasaini hao wanne ili waweze kueleza matumizi ya kiasi hicho cha fedha walichoidhinisha hundi na kulipwa kwao katika nyakati tofauti.

**UBADHIRIFU FEDHA**

Hasunga alisema uhakiki wa taarifa ya kibenki ya akaunti Na. 22606600144 ya mfuko huo Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni kwa kipindi kinachoanzia Julai 2018 hadi Novemba 2021, ulibaini Sh. milioni 28.2 kililipwa kwa wanufaika sita kupitia akaunti zao binafsi, hivyo Jeshi la Polisi lilitakiwa kuchukua hatua stahiki dhidi ya Erasto Mtweve na kurejesha kiasi hicho kutoka kwa wanufaika.

Aliwataja wanufaika hao kuwa ni Msanga Juma Rajabu, Joseph Mikongoti, Motomoto Erasto Kilasa, Nyamya Lameck Norbert, Msengi Boniface Martin na Joseph Beda. Walishiriki katika ubadhirifu wa kiasi hicho.

Alisema ukaguzi ulibaini Hamza Khamis Haji, aliyekuwa Mkaguzi Msaidizi, E.2350 SGT Abdalla Said Abdalla na F.2061 CPL Makame Ismail Mohamed kwa pamoja walishirikiana kufanya udanganyifu katika kuhuisha akaunti Na. 22901603799 kwa lengo la kuwezesha ubadhirifu huo na kusababisha hasara ya Sh. 988,450,000 kwa mfuko.

Hasunga alisema ukaguzi ulibaini Sh. 511,500,000 kati ya Sh. 576,500,000 zilizolipwa, hazikuwafikia walengwa (askari/warithi wa askari aliyefariki) baada ya walipwaji PF. 21751 A/Insp. Hamza Haji na H.6450 PC Suleiman Khamis Mohamed kushindwa kuthibitisha matumizi ya fedha hizo.

Vilevile, alisema ukaguzi ulibaini watiasaini na walipaji WP. 9980 SGT Amina Abdalla Ameir, E. 7416 D/SGT Khamis Abdalla Shaka na PF 18538 Inspekta Ally Hassan Zyuma wanawajibika katika ufujaji wa Sh. 306,000,000 zisizothibitika matumizi yake.

Pia alisema hakukuwa na maelezo kuhusu matumizi ya Sh. 24,946,000 na matumizi ya Sh. 15,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya dizeli hayakubaliki kufanyika kwa fedha za mfuko huo na pia hayakuthibitika kufanyika kwa kuwa hakukuwa na nyaraka za ununuzi wala matumizi ya mafuta hayo.

Hasunga pia alisema timu ya ukaguzi ilibaini kuwa mfuko huo haukuwahi kukaguliwa tangu mwaka 2018/19 hadi 2020/21 baada ya kuombwa kuwasilisha taarifa zilizokaguliwa kupitia barua yenye Kumb. Na. CTA.35/364/01D/90 ya Januari 11 mwaka 2022.

Alisema ASP. Yusta Andrew Mwasanyamba, aliyekuwa Meneja wa mfuko huo kuanzia Julai 2018 hadi Februali 2020 hakueleza sababu zilizopelekea kutokaguliwa kwa mfuko.

Hasunga alisema ukaguzi pia ulibaini malipo kwa wanufaika watatu wasiotambulika na Jeshi la Polisi, kwamba wahusika hao walijihusisha na malipo kwa watu wasiokuwa polisi.

Alisema taarifa ya ofisa masuuli imebainisha kuwa Jane John Mganga, CPL John Kaposwe Erasto Mtweve, Mahuna Salehe Koshuma na Maridadi Halima Hemed walifukuzwa kazi na kesi yao inaendelea katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Hata hivyo, SGT Deus John Shija alistaafu kazi Julai Mosi 2021 na hadi sasa hajachukuliwa hatua za kisheria licha ya kutorejeshwa Sh. 759,192,010 za mfuko huo baada ya kuazimwa na matumizi ya Sh. 855,838,668 kutothibitika

Hasunga alisema taarifa ya ukaguzi imebainisha kuwa ACP Leonard Bonaventura Ngassa, Mkuu wa Fedha wa Jeshi la Polisi alibainisha kuwa jeshi hilo lilirejesha Sh. 232,256,508 kati ya Sh. 991,448,518 kilichoazimwa na Jeshi kutoka katika mfuko huo.

Alisema uhakiki wa vielelezo vilivyowasilishwa ulibaini kuwa Sh. 759,192,010 hakikuwa kimerejeshwa kama ilivyobainishwa.

Hasunga alisema: "Ilibainika kuwa matumizi ya Sh. 855,838,668 ya fedha zilizoazimwa hayakuthibitika usahihi na uhalali wake kwa kuwa hakukuwa na vielelezo stahili vilivyowasilishwa."

Katika hatua nyingine, akichangia taarifa hizo za kamati bungeni jana, Mbunge wa Busega (CCM) Simon Lusengekile alitaka kufanyike ukaguzi wa kiuchunguzi kwa Kampuni ya Mafuta ya TANOIL ili wote waliohusika na hasara ya Sh. bilioni 7.8 wajulikane na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mbunge wa Viti Maalum, Conchesta Rwamlaza aliwataka watendaji wa halmashauri nchini kuacha roho mbaya. Wawalipe wazabuni wanaowadai.

Mbunge wa Lulindi (CCM), Issa Mchungahela alisema tatizo kubwa ya taifa ni watu wake kukosa uzalendo. Wajitathmini.

Alisema kumekuwa na shida ya upoptevu wa maadili katika taasisi mbalimbali na kuwa katika mahojiano ya taasisi nyingi amebaini maofisa masuhuli wengi hawatambui majukumu yao au kwa makusudi wameamua kutoyatekeleza.

Mbunge wa Mtoni (CCM), Abdulhafar Idrissa Juma alitaka serikali kuboresha hatua za kinidhamu zinazochukuliwa kwa watendaji wabadhirifu.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Suma Fyandomo alisema halmashauri zina wakurugenzi ambao siyo waaminifu. Serikali ilianzisha utaratibu wa 'force account' kwa nia njema, lakini halmashauri zingine zinafanya vibaya.

HABARI KITAIFA



Mkurugenzi wa Sheria wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), Florence Yamati (wapili kushoto) akitiliana saini mkataba na Mwakilishi wa Kampuni ya Sinohydro Corporation Ltd (wa pili kulia) katika ofisi za DAWASA mkoani Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kujenga miundombinu ya maji. Katikati ni Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mwinyi: Hospitali za wilaya kuwa na huduma za kisasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa hospitali zote 10 za wilaya Unguja na Pemba zitakuwa na huduma bora za afya za kisasa pamoja na mahitaji muhimu ikiwamo ya chakula kwa wagonjwa.

Aliyasema hayo katika mwendelezo wa ziara zake katika shamrashamra za kutimiza miaka mitatu ya uongozi wake wakati akifungua Hospitali ya Wilaya Wete Pemba, iliyopo Kinyasini.

Alisema hakuna haja tena ya familia za wagonjwa kubeba chakula kwa ajili ya ndugu zao ambao wamelazwa hospitalini wakati wakipatiwa matibabu kwa sababu mlo kamili utapatikana bure katika hospitali hizo.

"Simuombei mtu aumwe aingie katika hospitali hii, lakini kuna mambo mazuri sana, tumieni huduma zilizopo yale matatizo tuliyokuwa nayo kipindi cha nyuma ikiwamo kukosa dawa sasa hivi tatizo hilo halipo tena, vipimo vyote mtavipata, lakini hata chakula ikiwamo maandazi, mayai na chai ya maziwa mtakipata hospitalini hapa, awali mambo hayo hayakuwapo mlikuwa mkipewa wali tena mchele unaotumika ni zile chenga za kupikia vitumbua," alisema.

Alisema lazima wafanyakazi wa afya wahakikishe kuwa wanatoa huduma bora kwa wananchi wanaofika katika hospitali hiyo, lakini pia kujifunza mbinu mpya kutoka kwa wataalamu bora ambao watatoa huduma katika hospitali hizo ili nao wawe na uwezo wa kutoa huduma.

Aliwatoa hofu wafanyakazi wa hospitali hizo kutokuwa na wasiwasi na maslahi yanayozingatiwa ili kutoa huduma bora na kuendelea na moyo wa kujitolea kuwa na bashasha kwa wagonjwa.

Aliwataka waendeshaji wa hospitali hizo ambazo ni taasisi binafsi kutoa huduma za afya zinatolewa kwa muda wa saa 24 na wananchi wapate huduma za maabara kwa haraka.

"Tukiyafanya yote hayo bila shaka hospitali hizi zitakuwa mfumbuzi mkubwa wa matatizo yetu ya afya kwa miaka mingi na upasuaji mwingi utafanyika hapa," alisema.

Aliwataka wananchi kutumia huduma katika hospitali hizo na hakuna sababu ya kutokwenda hospitali kupata matibabu kwa sababu huduma zote muhimu zitapatikana.

Kadhalika, huduma hizo zitatolewa bure na serikali anayoingoza na ndiyo itakayolipia gharama hizo na kwamba ni vyema kuzitunza hospitali hizo.

Akizungumzia fidia kwa wananchi ambao wamechukuliwa maendeleo yao kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maendeleo, Dk. Mwinyi alisema hakuna atakayedhulumiwa au kuonewa na kila mmoja ambaye eneo lake limechukuliwa kwa ajili ya shughuli hizo atalipwa fidia.

"Bado tuna mambo mengi ya kujenga hivyo wananchi msiwe na wasiwasi pale ambapo eneo tutalihitaji fidia kamili mtalipwa, na nimuagize mkuu wa mkoa kwamba wananchi wote ambao hawajalipwa fidia katika eneo hili lilojengwa hospitali niorodheshee majina yao unileteee," alisema.

Naibu Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh, alisema, huduma za afya kisiwani Pemba hivi sasa zimeimarishwa na huduma zote muhimu zinapatikana ikiwamo ya dharura wakati hapo awali Pemba hakukuwa na chumba maalum kwa wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum (ICU).

Alisema kuwa sasa Zanzibar ina uwezo wa kudhibiti vifo visivyokuwa vya lazima na kwamba ni vyema watendaji wa afya wakaendelea kutoa huduma bora kwa wananchi.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema ujenzi wa hospitali hiyo unatokana na fedha za kupunguza makali ya Uviko-19, zilizotolewa na WIF na umegharimu zaidi ya Shilingi milioni saba kwa ujenzi wa ununuzi wa vifaa.

Alisema hospitali hiyo inatoa huduma kwa ngazi za wilaya na imeanza kazi Oktoba 6, mwaka huu na huduma zinazotolewa ni za kiwango kikubwa zenye uwezo wa kulaza wagonjwa 100 kwa wakati mmoja.

Alisema hospitali hiyo itasaidia utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi wapatao 18,712 wa wilaya hiyo ya Wete na ina madaktari bingwa.

# Walimu wanaojitolea kutambuliwa rasmi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeandaa mwongozo wa kuwatambua walimu wanaojitolea katika shule zote nchini.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk.Festo Dugange, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mpanda Vijijini (CCM), Moshi Kakoso.

Mbunge alihoji serikali ina mkakati gani wa kuwapa ajira walimu wanaojitolea katika shule za msingi na sekondari ajira zinapotoka badala ya kuwaacha.

Akijibu, Dk. Dugange alisema Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeandaa mwongozo huo.

"Mwongozo umeipa Ofisi ya Rais -TAMISEMI jukumu la kuandaa mfumo wa walimu wanaojitolea. Kwa sasa Mfumo huo unaendelea kuandaliwa, utakapokamilika walimu watajulishwa ili waanze kufuata utaratibu wa kujisajili katika mfumo huo ili kurahisisha utambuzi wao," alisema.

Alisema serikali imeendelea kuajiri watumishi wote bila kuangalia wanaojitolea na wasiojitolea.

"Changamoto ya kuajiri walimu wanaojitolea ilitokana na utaratibu ambao haukuwa rasmi wa kuwasilisha majina ya walimu wanaojitolea kwasababu baadhi ya wakuu wa shule wasiowaamini walikuwa wanatumia fursa hiyo ya kuingiza majina ya walimu ambao hawajitolei na kuwaacha wanaojitolea," alisema.

Alisema kutokana na sababu hiyo serikali imeandaa mwongozo huo na mfumo ambao walimu wataingia na kujisajili wenyewe na itasaidia kuona waliojitolea kwa muda mrefu ili kupewa kipaumbele cha kupata ajira.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alitaka serikali kupitia TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Utumishi kujipangia muda ili suala hilo lijulikane litafanyika kwa muda gani na wanaojitolea wasikatishwe tamaa kuendelea kujitolea.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA Visaidizi vya Urambazaji/Vielelezo vya kusafiria baharini.**

**KUMB: ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0123**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta, yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta ghafi yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilichopo katika eneo la ufukwe wa bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa kilomita 2 kutoka ufukweni kutoka eneo maalumu la kuhifadhia mafuta kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

BESIX Ballast Nedam (BBN) Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, Ununuzi na Ujenzi wa Gati na Kituo Cha Upakiaji katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) linakaribisha Kampuni zenye uzoefu kueleza nia yao katika:

**Ugavi wa Visaidizi vya Urambazaji / Vielelezo vya kusafiria baharini (Aids to Navigation)**

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**

Ugavi wa Visaidizi vya Urambazaji / Vielelezo vya kusafiria baharini (Aids to Navigation) utahusisha:

- Kusanifu, Kutengeneza, na Ugavi wa Visaidizi vya Urambazaji / Vielelezo vya kusafiria baharini (Aids to Navigation).

Vipengee vinavyohitaji ni:

- Taa 9 za kusafiria baharini (LED, mwonekano wa Nm 3, Inayotumia nishati ya jua / Sola, imeidhinishwa na IALA)
- Taa 4 za kusafiria baharini za ATEX (mwonekano wa Nm 10, Inayotumia nishati ya jua / Sola, imeidhinishwa na IALA)
- King'ora cha Ukungu 1 (Msururu wa mihimili ya sauti ya Nm 2, Inayotumia nishati jua / Sola)

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Makampuni yenye nia yanaalikwa kutuma maombi yao kwa kuambatanisha vifuatavyo:

- Pendekezo la aina, ubora na upakaji wa nyenzo (coating of materials) zitakazotumika kutengeneza vifaa husika,
- Orodha ya uzoefu iliyo na historia/rekodi husika inayoonyesha uzoefu usiopungua miaka mitano (5) katika ugavi wa vifaa vya kusafiria majini,
- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali kutekeleza kandarsi husika.
- Sera ya Ubora, mazingira na usalama pahala pa kazi ya Kampuni na uthibitisho wa viwango vya ubora unaohitajika wa ISO au vyeti sawa;
- Hati ya mlipa kodi ya kampuni ya mwaka uliopita 2022
- Uthibitisho wa usajili wa biashara na leseni halali ya kufanya biashara kwa Tanzania.
- Kuzingatia kanuni za petroli za matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu kwa usemi huu wa maslahi unapendekezwa sana.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu wanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati husika kwa **procurement@bbnltd.co.tz** . **(Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: MB 20 & Hati zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza) mnamo au kabla ya tarehe 17 ya Novemba 2023 , Saa 1200 jioni, saa za Tanzania.**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini zaidi yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka:** Kampuni zilizokidhi mchakato wa awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

217696401



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma (kushoto), akiwasalimia wanufaika wa mfuko huo, alipowasili kwenye kikao kazi na wahariri wa vyombo vya habari, jijini Dar es Salaam jana. Kikao hicho kimeratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kutoa fursa kwa watendaji wa WCF kueleza utekelezaji wa majukumu na mafanikio ya mfuko huo miaka 8 tangu uanzishwe. Wengine ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Thobias Makoba (wa pili kushoto) na (wa tatu kushoto) ni Ofisa Mwandamizi wa Uhusiano wa Ofisi hiyo, Sabato Kosuri. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtoto wa Bilionea Msuya afichua mali alizokuwa akimiliki baba yake

**Na Grace Gurisha**

MTOTO wa aliyekuwa mfanyabiashara wa madini mkoani Arusha, marehemu Erasto maarufu kama Bilionea Msuya, Kevin Erasto Msuya, ameieleza mahakama kuwa baba yake mzazi alikuwa anamiliki gari moja tu.

Aidha, amedai kuwa baba yake hakuwa anamiliki mali jijini Dar es Salaam na Moshi na pia wakati wanafuatilia akaunti za benki, walikuta zimefungwa.

Kevin alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akitoa ushahidi wake wa kumtetea mama yake mzazi, Miriam Mrita, anayetuhumiwa kumuua wifi yake, Aneth Msuya, Mei 26, 2016 Kibada, Kigamboni mkoani

Alidai kuwa alifanya jukumu la kukusanya mali za marehemu baba yake yeye na dada yake, Grory Msuya, baada ya kupewa maelekezo ya kufanya hivyo na Mahakama Kuu Kanda ya Arusha kisha kuziwasilisha katika mahakama hiyo kama msimamizi wa mirathi.

"Mimi na dada yangu Grory tulikwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa lengo la kujua kama magari ambayo baba alikuwa akiyamiliki au yaliyobadilishwa umiliki kutoka jina la baba kwenda kwa mtu mwingine. Tulibaini baba alikuwa akimiliki gari moja tu," alidai Kevin.

Pia alidai kuwa aligawana majukumu na dada yake pamoja na wakili, ambapo walikwenda kwenye Halmashauri za Arusha, Moshi na Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya kujua kama baba yao alikuwa anamiliki ardhi.

"Tuligundua Dar es Salaam na Moshi baba hakuwa anamiliki ardhi na pia hatukubaini kama kulikuwa na ardhi ambayo baba alikuwa anamiliki halafu ikabadilishwa umiliki kwenda kwa mtu mwingine," alidai.

Shahidi huyo ambae alisimama kizimbani kama msimamizi wa mirathi ya baba yake, alidai kuwa Arusha ndiko walikuta baba yao anamiliki ardhi pamoja na nyumba mbalimbali. Pia alidai kuwa hawakukuta mali iliyobadilishwa jina kutoka jina la baba yake kwenda kwa mtu mwingine.

"Kazi iliyofuata ilikuwa kufanya uchunguzi kuangalia kama kuna kampuni ambazo baba alikuwa anamiliki hisa. Tulibaini ana kampuni mbili, moja ana hisa 600 na nyingine ana hisa 400. Za mama sikumbuki kwa sababu nilikuwa nashughulikia hisa za baba," alidai.

Akiendelea kuongoza na Wakili Peter Kibatala, anayemtetea mama yake, Kevin alidai kuwa baada ya kujua mali hizo waliziorodhesha kwenye karatasi vikiwemo viwanja, magari, nyumba na kwamba kufanya hivyo lilikuwa sharti la mahakama.

"Zoezi lilifuata ni kugawanya mali kwa wanufaika, tuliorodhesha kwenye karatasi baada ya hapo mimi na Grory tuliwaita wadogo zetu, Maurine na Cavin, tukawaeleza tumekusanya mali za baba na tumezigawa hivi. Walikubaliana na mgawo huo. Mama hatukuweza kumfikia kwa sababu alikuwa gerezani," alidai.

> "Mimi na dada yangu Grory tulikwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa lengo la kujua magari ambayo baba alikuwa akiyamiliki au yaliyobadilishwa umiliki kutoka jina la baba kwenda kwa mtu mwingine. Tulibaini baba alikuwa akimiliki gari moja tu," alidai Kevin.

Alidai kuwa baada ya kumaliza hapo nyaraka za ukusanyaji wa mali na za mgawanyo walizifaili mahakamani kama walivyoelekezwa na mahakama.

Pia alidai kuwa bibi (Ndeshukulwa na babu (Elisaria) waliamua kuwapa ardhi licha ya kwamba si wanufaika na hiyo ilitokana na upendo wao kwao na hata walipoulizwa mbele ya mahakama hawakuwa na dukuduku na walisema haina tatizo na wamefurahi.

Alidai kuwa baada ya Jaji Kamuzora kumhoji mtu mmoja mmoja na kujiridhisha kwamba hakuna tatizo, Agosti 11,2022 alifunga mirathi.

Awali, Dereva mshitakiwa namba moja, Miriam, Karim Mruma, alidai kuwa yeye ndiye dereva wa tajiri huyo na kila sehemu anayotaka kwenda huwa anamweleza.

Pia alidai Mei, 2016 bosi wake hakuwahi kusafiri kutoka nje ya mkoa wa Arusha lakini pia kuna kipindi mshtakiwa huwa anaendesha gari yeye peke yake, kwa hiyo hawezi jua huwa anakwenda wapi.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi kesho saa 3:00 asubuhi ambapo Kevin ataulizwa maswali ya dodoso na jopo la mawakili wa serikali, Paul Kimweri, Yasinta Peter, Generosa Montana na Marietta Maguta.

Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji hayo ya wifi yake, Aneth Msuya, aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake, Kibada Kigamboni , Dar es Salaam, alikiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo. Mshitakiwa wa pili anaitwa Revocatus Muyela.

## WCF yaorodhesha majanga inayowafidia wafanyakazi

**Na Mwandishi Wetu**

WAAJIRI nchini wametakiwa kujiunga na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) ili kuondoa migogoro baina yao kwa kuwapa mafao bila kikomo baada ya kupata ulemavu, kuugua na kufariki dunia, wakiwa kazini

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, wakati akizungumza katika kikao kazi na wahariri na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu kwa taasisi zilizopo chini yake kuelezea umma mafanikio, changamoto wanazokabiliana nazo na matarajio katika utekelezaji wa majukumu yao.

"WCF ni moja ya mifuko ya hifadhi za jamii nchini ambao umeanzishwa kwa sheria ya fidia kwa wafanyakazi sura namba 263... kwa mujibu wa sheria, kila mwajiri nchini anapaswa kujiunga na WCF," alisema Dk. Mduma.

Aliyataja mafao hayo kuwa ni pamoja na kipindi ambacho mfanyakazi aliyeugua akiwa kazini atakuwa akipatiwa matibabu hadi atakapopona.

Ulemavu wa muda, fao ambalo limekuwa likitolewa wakati mwanachama akiwa anapatiwa matibabu hadi itakapothibitishwa na daktrari kuwa amepona.

Kwa mujibu wa Dk. Mduma, wanatoa fao la ulemavu wa kudumu kwa mwanachama wao ambaye hawezi kupona tena baada ya kuumia akiwa kazini.

"Fao la kumuuguza mgonjwa nalo linatolewa na mfuko wetu kwa mtu atakayeteuliwa na si vinginevyo," alisema.

Alitaja fao jingine kuwa linatolewa kwa wategemezi wa mwanachama wao aliyekumbwa na majanga hayo akiwamo mwenza kama yupo na watoto.

"Kama mwenza yupo atapatiwa fao hilo baada ya mumewe kufa, na kama hayupo basi watoto," alisema.

Akizungumzia fao la ulemavu wa kudumu, alisema mwanachama wao atapatiwa mafao yake kila mwezi hadi atakapofariki dunia, kisha wategemezi wake.

Alisema fao la mazishi, nalo ni miongoni mwa mafao saba yanayotolewa na mfuko huo baada ya wanachama wao kufariki dunia na la saba ni la utengemaa kwa mwanachama aliyepotoza viungo kuwekewa vya bandia.

Awali, alisema mfuko huo unajiendesha kwa fedha inazokusanya kutoka katika vyanzo vyake, ikiwamo michango ya waajiri ya wafanyakazi wao, miradi ya uwekezaji, faini inazotoza waajiri wanaochelewesha kuwasilisha michango na gawio kutoka serikalini.

Mkurugenzi Uzalishaji wa WCF, Anselim Peter, akiwasilisha mada ya mafao ya fidia kwenye kikao hicho, alisema ni wajibu wa mfuko huo kulipa fidia kwa wanachama wao waliopata ajali ili kulinda nguvu kazi ya taifa, kupunguza umaskini na kuondoa migogoro baina ya mwajiri na mfanyakazi.

Peter alisema, mfuko huo huanza kulipa mafao baada ya mwanachama wao kupata ajali, kutoa aina zote za matibabu bila kujali kiwango cha uchangiaji.

Alitoa mfano wa bwana shamba aliyejeruhiwa jicho wakati akitekeleza majukumu yake kuwa WCF walimpeleka India kwa matibabu na kugharimia Sh. milioni 150, kiwango ambacho hakilingani na mchango kwenye mfuko huo.

Alisema mfuko huo, pia uligharamia zaidi ya Shilingi milioni saba kwa ajili ya kumfanyia upasuaji wa mguu kijana hospitalini mara saba.

Mkurugenzi Tathimini wa WCF, Dk. Abdulsalaam Omar, akizungumzia kuhusu visa halisi katika mfuko huo, alimtaja Halima Sheik Mbwana, ambaye alikatika mkono wakati akiwaokoa abiria baada ya basi alilokuwa akiendesha kupinduka akisema mfuko huo umegharamia matibabu na kuwekewa mkono wa bandia.

Alisema Hassan Sim Jambau, madaktari wamemuwekea mguu wa bandia baada ya mfupa wake kusagika kwa kupata ajali wakati akienda kazini.

Mnufauka mwingine wa mfuko huo, Beauty Michael Lameck, anapewa mafao baada ya mumewe kufariki dunia kwa ajali ambayo ilisababisha kukatika miguu yote mwili.

Anasema mbali na kupata mafao hayo na watoto wake, pia mfuko huo ulitoa Sh. 400,000 kama rambirambi za mazishi ya mumewe.



Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Umoja wa wakulima na Uhifadhi wa Mazingira (UWAMAKIZI) wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Hassani Shakaza (kulia) akikabidhi msaada wa mbegu za Karafuu kwa mmoja wa wakulima wa Tarafa ya Amani, juzi. Taasisi hiyo, tayari imeshakabidhi miche 6000 ya karafuu kwa wakulima kwa ajili ya kupanda katika mashamba yao. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mbunge ashtukia jambo kanuni za mipango miji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA



MBUNGE wa Njombe Mjini, Deodataus Mwanyika (CCM) ameitaka serikali kufanya marekebisho ya kanuni za mipango miji ili maeneo ya miji yenye sura ya vijiji yasitawaliwe na sheria za miji.

Alitoa kauli hiyo bungeni jana alipouliza swali la nyongeza, akisema uhalisia uliopo ni kwamba kuna mkanganyiko mkubwa kwenye halmashauri za miji ambazo zina vijiji.

"Waziri atakubaliana na mimi kuwa ni wakati sasa wa kutoa maelekezo kwa sababu sheria inataka utayari wa eneo kabla ya kutangazwa kuwa eneo la kuendelezwa kimji, maeneo mengi yametangazwa kuwa maeneo ya kuendelezwa kimiji kabla ya utayari.

"Sasa Waziri (Jerry Silaa) uko tayari kutoa maelekezo ili kufanyika marekebisho ya kutangaza maeneo ya vijiji yasitawaliwe na sheria za miji?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa alisema tayari serikali imesimamisha matumizi ya kanuni hizo na kutoa maelekezo kwa wataalamu kuipitia.

Alilithibitishia Bunge kuwa kanuni hiyo wameisimamisha na kutoa maelekezo kwa watalaamu wa ardhi wa Wizara ya Ardhi kuipitia upya ili iendane na hali halisi ya maeneo husika.

"Kanuni hii ndiyo inahusika katika ujenzi wa vituo vya mafuta vinavyochukua ardhi kidogo na mashamba ya mijini ya ekari tatu.

"Kwa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, Mji wa Njombe ni mji wa kilimo cha parachichi na sisi Wizara ya Ardhi hatuwezi kuwa kikwazo kuendeleza zao la parachichi na tutamshirikisha mbunge (Mwanyika) na wabunge wengine wenye maeneo ya miji yenye sura za vijiji," alisema.

Katika swali la msingi, Mwanyika alitaka kujua sababu za serikali kutumia sheria za ardhi zinazokusudiwa kutumika kwenye miji maeneo ya vijijini.

Akijibu swali hilo, Silaa alisema mfumo wa kisheria wa usimamizi wa ardhi nchini umegawa ardhi katika makundi matatu ambayo ni Ardhi ya Kijiji, Ardhi ya Hifadhi na Ardhi ya Jumla.

Alisema kwa kuzingatiwa mgawanyo huo, Ardhi ya Vijiji inasimamiwa na Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura 114 na maeneo ya miji yanasimamiwa na Sheria ya Ardhi, Sura 113.

Hata hivyo, yapo baadhi ya maeneo ndani ya mipaka ya vijiji yanayosimamiwa na Sheria ya Ardhi, Sura 113 kutokana na kumilikishwa kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura 114 au kuhawilishwa.

Alisema baadhi ya maeneo ya vijiji yametangazwa kuwa ya kuendelezwa kimji na kuandaliwa Mpango Kabambe na hivyo kuyafanya yasimamiwe na Sheria ya Ardhi, Sura 113.

# Watumishi 14 wachunguzwa tuhuma wizi wa milioni 66/-

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) inawachunguza watumishi wa afya 14 wa Manispaa ya Temeke kwa madai ya kuchezea mfumo wa Bima ya Afya Jamii Iliyoboreshwa (iCHF) na kujipatia Sh. milioni 66.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Temeke, Holle Makungu, alisema watumishi hao walisimamishwa kazi hivi karibuni ili kupisha uchunguzi dhidi ya tuhuma zinazowakabili.

"Tunafanya uchunguzi wake ili ukikamilika na tukijiridhisha wamefanya hujuma hiyo tutawapeleka mahakamani. Uchunguzi umeanza hivi karibu, lakini huko nyuma kulikuwa na kamati imepita kuangalia mambo hayo. Ni kweli uchunguzi unaendelea. Fedha ni Sh. milioni 66," alisema.

Juzi usiku kulisambazwa video fupi katika mitandao ya kijamii ikiwaonesha watumishi hao wakiwa katika kikao na uongozi wa Manispaa ya Temeke, wakitajwa majina yao na kusimamishwa. Baadhi walikiri na wengine kuangua vilio.

**CAG, WATAALAMU**

Ripoti ya Uwajibikaji ya Viashiria vya Rushwa, Ubadhirifu na Udanganyifu 2021/22 iliyoandaliwa na Taasisi ya WAJIBU kutokana na ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za ukaguzi wa Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Mamlaka ya Serikali za Mitaa za mwaka wa fedha 2021/22, inabainisha miamala mbalimbali yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu wa fedha za umma.

Kwa mwaka wa fedha 2021/22, uchambuzi umeonesha kuna viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika matumizi ya kawaida, mishahara, mafao na rasilimali watu yenye thamani ya Sh. bilioni 411.31 yaliyotokana na kasoro mbalimbali.

Dosari hiyo imepungua kwa asilimia 63 kutoka Sh. trilioni 1.14 mwaka wa fedha 2020/21 mpaka Sh. bilioni 411.31 mwaka wa fedha 2021/22.

Mathalani, katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa (halmashauri), kasoro zaidi zilizobainishwa kuwa na viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu ni pamoja na halmashauri 19 zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 14.02 nje ya mpango wa ununuzi wa halmashauri husika.

Ni tatizo linaloonekana kuongezeka ingawa idadi ya halmashauri imepungua. Kwa mwaka 2020/21, halmashauri 24 zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 3.84 bila kuzingatia mpango wa ununuzi wa halmashauri husika.

Pia upo ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 7.45 ulifanyika katika halmashauri 45 za serikali za mitaa bila kuitisha nukuu za ushindanishi wa bei.

Baadhi ya Mamlaka ya Halmashauri zilizokuwa na kiasi kikubwa ni pamoja na: Wilaya ya Kaliua Sh. milioni 894.82, Wilaya ya Missenyi Sh. milioni 648.60, Wilaya ya Bunda Sh. milioni 576.04 na Wilaya ya Momba Sh. milioni 445.07.

Kuna tatizo lingine la mikataba iliyotiwa saini bila kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali yenye thamani ya Sh. bilioni 6.68 kwenye halmashauri 20.

Upungufu pia ulionekana katika dhamana za utendaji wa mikataba ya miradi ya ujenzi yenye thamani ya Sh. bilioni 7.64 katika halmashauri 10. Mfano wa upungufu huo ni kuwapo dhamana ya utendaji uliyoisha muda wake katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# WCF uchangamkiwe na waajiri kulinda wafanyakazi wake

**MFUKO** wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) unaokoa wafanyakazi wengi wanaopata majanga wakiwa kazini, hivyo ni muhimu waajiri wakajiunga ili waajiriwa wao waweze kufaidika na mafao yanayotolewa na mfuko huo.

Kama ilivyo kwa mifuko mingine ya hifadhi ya jamii, mfuko huu unatoa mafao kwa mfanyakazi aliyepata majanga akiwa kazini pamoja na familia yake mpaka siku atakapoondoka duniani.

Mfuko huu ni taasisi ya hifadhi ya jamii iliyoundwa kwa mujibu wa sheria ya fidia kwa wafanyakazi sura 263.

Ulianza rasmi Julai Mosi, 2015 ukiwa na lengo la kuilinda jamii dhidi ya majanga kwa kulipa mafao ya pensheni, afya na fidia.

Kwa waajiri, mfuko huu una manufaa makubwa kwa sababu mfanyakazi anapopata ajali sehemu yake ya kazi na pengine akapata ulemavu wa aina yoyote, mfuko huu humlipa mafao yatakayomwezesha kujiendesha kimaisha bila kuwa tegemezi.

Vile vile, humsaidia mwanachama wake kwa kumpatia matibabu na kiungo cha bandia ambacho kitamsadia kuendelea na shughuli zake.

Tunasema ni muhimu kwa waajiri kujiunga na mfuko huu kwa sababu faida zake ni kubwa na humsaidia mfanyakazi aliyepata majanga kuishi bila kuwa na changamoto ya kimaisha.

Tumeshuhudia baadhi ya wafanyakazi waliokuwa na maisha mazuri, lakini baada ya kupata changamoto ya kupata ajali na kupoteza moja ya kiungo, wanabaki wakihangaika na familia zao kwa sababu mtu waliyekuwa wakimtegemea hawezi tena kufanyakazi.

Mfuko huo kwa sasa una uwezo wa kujiendesha kutokana na michango kutoka kwa waajiri wanachama wa mfuko huo ikiwa ni chanzo chake cha kwanza cha mapato na vile vile chanzo kingine ni kupitia uwekezaji uliofanya wa zaidi ya Sh. milioni 600 ambao umewezesha kupata mapato ya zaidi ya Sh. bilioni 300 kwa mwaka huu (2023).

Mafao yanayotolewa na mfuko huu ni pamoja na matibabu, ulemavu wa muda, ulemavu wa kudumu, kumuuguza mgonjwa, malipo kwa wategemezi, msaada wa mazishi na fao la utengemao.

Tofauti ya WCF na mifuko mingine ya hifadhi ya jamii, mfuko huu pamoja na kutoa mafao, lakini unatoa mafao ya matibabu.

Mfuko huo mpaka sasa umeshalipa fidia kwa wanachama wake zaidi ya Sh. milioni 60 na wapo ambao wamezalisha madai na kupokewa na WCF yanayofikia 18,782.


Mwelekeo wa WCF ni kuboresha huduma zake kwa kupanua wigo wa huduma za utengamao kwa kulipia huduma za mafunzo ya ujuzi mbadala (vocational rehabilitation).

Pia kuimarisha ushirikiano wa kiserikali na taasisi mbalimbali za serikali katika kutatua changamoto za kupokea taarifa zilizo sahihi za madai na michango, taasisi hizo ni pamoja na Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Mapato (TRA), Msajili wa Kampuni (BRELA) na mifuko mingine ya hifadhi ya jamii.

Pia kuimarisha upatikanaji wa huduma za mfuko katika mikoa mbalimbali nchini ikiwamo kupitia ufunguzi na uboreshaji wa ofisi za mfuko mikoani.

Mikakati ya WCF ni uthibitisho kuwa mfuko huo uko vizuri kwa ajili ya kuhakikisha jamii inafaidika na mafao yanayotolewa na mfuko huo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

Na Mary Seme

# Kwenye hili analoliendeleza kukuza utalii kitaifa, iko wazi 'Mama kaupiga mwingi'

Utalii ni hazina muhimu ya kiuchumi na biashara katika maendeleo ya nchi. Mataifa mengi yanajikita katika ukanda wake kuungana na aina ya utajiri wa asili iliyo nayo. Hata hivyo, utalii wa viumbe na mimea ya asili, ndio bado inaonekana kushika nafasi pana katika soko la sekta hiyo.

Ni eneo ambalo Tanzania imebahatika kumiliki kuwa na vituo vya wanyama, milima na mimea. Leo hii ukiutaja Mlima Kilmanjaro nchini, basi inaangukia katika utajiri asili wa yanayomilikiwa na serikali nchini, huku upande wa pili kukiwapo wanyama. Vyote hivyo kwa jumla wake, vinaangukia tafsiri ya mapana ambayo nchi imejaliwa kihistoria, ikijumuishwa na nyendo za amani na utulivu tangu hata kabla ya kupatikana uhuru, aina ya ukombozi wake kufikia uhuru, haukuhusisha mapigano au kumwaga damu.

Naam! Katika wajihi huo wa kiutalii, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, mara alipoamua kuwekeza nguvu na mikakati yake katika mifumo uchumi na biashara baada tu ya kukabidhiwa dhamana ya kuongoza, basi sekta ya utalii ilichukua nafasi yake. Mkuu huyo akaanza jukumu la utendaji kwa kushiriki binafsi sinema ya Royal Tour, ambayo sasa sote tunijua. Leo hii sifa ya sinema hiyo, kimataifa nchi inaonyesha kung'ara katika sekta hiyo, wana fani wakikiri kasi ya ongezeko. Katika lugha rahisi, naye kaamua kuweka mchango wake wa mfano katika kukuza biashara ya utalii nchini.

Ni dhana ya ubunifu wake Rais Dk Samia, akisisitiza kutanuliwa na hata kugusa maeneo mengine kisekta ambayo hayakuguswa au kuhusianishwa na utalii, mathalan juhudi ambazo zinaendeshwa kitaifa kukuza maradufu wigo na ujuzi katika stadi za tiba kupitia hospitali kubwa, kama vile Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete na Taasisi ya Mifupa na Mishipa Fahamu Muhimbili (MOI), sasa zikipata wageni wa nje kuja kupata ujuzi wa kidaktari, hali kadhalika wapo wanaotibiwa. Hapo inaangukia sasa katika dhana ya utalii tiba.

Ilikuwa jambo la kuvutia, pale tuliposhuhudia takwimu kitaifa la ongezeko la watalii likiongozwa na Marekani, ambako kwao Rais Dk. Samia akashiriki kuunda sinema hiyo, kisha ikazinduliwa kitaifa jijini Arusha Tanzania. Ni matunda ya juhudi za moja kwa moja kutoka kwa mkuu huyo wa nchi, akiacha somo ngazi ya chini kwamba, hilo liendelezwe katika staili nyingi kufanikisha matunda ya sekta utalii.

Nilifurahishwa sana kuona anachokibuni rais, sasa kinashuka waliko wananchi, pale kiongozi mmoja wa kimani akatamka hata matendo na mahubiri mema kwa Mungu yanapofanyika nchini vizuri na kwa mafanikio, tutakuwa tunatenda ya kiimani na wakati huohuo tunabuni anachokiita 'Utalii Imani' watu wakifika nchini kuabudu kwa mafanikio.

Ni darasa hata kwa viongozi wa ngazi mbalimbali za chini kujiuliza, wao wana mchango gani katika kufanikisha utalii na sekta nyinginezo zinazoambatana nazo kama vile biashara mbalimbali zinazohudumia utalii; hoteli, usafiri na wanaowaongoza watalii? Hapo inaleta majibu katika sura nyingi sana kama vile kodi kwa serikali, wigo wa ajira, masoko mbalimbali yanayoambatana nayo.

Daima mafanikio ya nchi hayapatikani kwa mkono mmoja, rais na viongozi wa juu wao nao wana wajibu wao kuonyesha njia, ingawaje Dk. Samia akavuka hatua zaidi, kwa kushiriki njiani. Sehemu ya umma uliobaki ndio watendaji wakuu wakiwa wawajibikaji katika kile wanachoonyeshwa na mamlaka hiyo kuu, ambayo umma ukiungana nao vizuri, inafungua njia zaidi kuata dhana maendeleo.

Taaluma zinatueleza, maendeleo ni tunda la mabadiliko kutoka ngazi ya chini kupiga hatua zaidi ya kuendelea. Ili kiuendelea, kunahitajika juhudi na mikakati kupafikia huko kwa ufanisi.

Ndicho alichokifanya na anendelea kukifanya Dk. Samia. Mimi na wewe tujiulize, tunamuungaje mkono mkuu huyo wa nchi, tena katika bahari ya kijamii. Amesimama mwana mama mlezi wa familia, ambaye kaipa kipaumbele sekta ya utalii, wakati wa kuamua ndio huu, kila Mtanzania kwa nafasi yake.

# Mshauri Kodi apandishwa kizimbani mashtaka hasara ya mamilioni TRA

**Na Grace Gurisha**

MSHAURI wa Kodi, Denis Tililo (29) amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam akikabiliwa na mashtaka manane likiwamo la utakatishaji na kuisababishia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hasara ya Sh. milioni 118.9.

Tililo ambaye ni mshauri wa kodi wa kujitegemea, mkazi wa Msingwa, Dar es Salaam, alisomewa mashtaka yake na Wakili wa Serikali Theresia Mtao aliyesaidiana na Auni Chilamula na Emmanuel Medalakini kutoka TRA mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rehema Lyana.

Mtao alidai kuwa katika kesi hiyo mshtakiwa anakabiliwa na mashtaka sita ya kutoa risiti za uongo kutoka kwenye mashine ya kielektroniki (EFD), kuisababishia TRA hasara na utakatishaji fedha zaidi ya Sh. milioni 100.

Alidai kuwa Agosti 28 mwaka huu, maeneo ya Buguruni ndani ya Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, mshtakiwa Tililo alitoa risiti ya uongo kutoka kwenye mashine ya EFD iliyosajiliwa kwa jina la Yasini Revelian kwa nia ya kumdanganya Kamishna Mkuu wa TRA kwa ajili ya kumlipa mfanyabiashara hewa aitwaye Janeth Kitego mwenye namba ya Mlipakodi (TIN) 43-472-604 Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya Sh. milioni 7.6.

Mshtakiwa huyo pia anadaiwa kutoa risiti ya uongo yenye namba 342 kutoka kwenye mashine ya EFD iliyosajiliwa kwa jina la Revelian kwa lengo la kumdanganya Kamishina Mkuu kumlipa Kitego VAT ya Sh. milioni 30.5.

Mshauri huyo wa kodi anadaiwa kutoa risiti ya uongo namba 343 kutoka kwenye mashine hiyo iliyosajiliwa kwa jina la Revelian na kumdanganya Kamishna Mkuu kumlipa Kitego VAT ya Sh. 27,457,627.12.

Mtao alidai Tililo alitoa risiti ya uongo ya namba 343 kupitia mashine hiyo ya EFD ya Revelian kwa lengo la kumdanganya Kamishna Mkuu kuwa anamlipa mfanyabiashara hewa ambaye ni Kitego mwenye TIN namba 143-472-604 VAT ya Sh. milioni 27.4/-

Katika mashtaka mengine, inadaiwa mshtakiwa alitoa risiti ya uongo namba 344 kwa kutumia mashine hiyo yenye kiasi cha Sh. milioni 780 na kupotosha mfumo wa kodi wa TRA kwa lengo la kumdanganya kamishna ili kumlipa Kitego VAT ya Sh. 118,983,050.85.

Ilidaiwa kuwa kwa makusudi mshtakiwa aliisababishia TRA hasara ya Sh. milioni 118.9 kwa kutoa risiti za uongo ambazo zilikuwa zinalenga kutoa taarifa za uongo kwa Kamishna pamoja na mfumo wa mamlaka hiyo.

Katika shtaka la utakatishaji fedha, Tililo anadaiwa kufanya miamala ya fedha ya Sh. 118,983,050.85 wakati akijua kuwa fedha hizo ni zao la makosa la uhalifu la kutumia risiti zisizo halali.

Kwa mujibu wa upande wa mashtaka, upelelezi wa kikodi katika kesi hiyo haujakamilika, hivyo umeomba mahakama kupanga tarehe nyingine kwa ajili ya kesi hiyo kutajwa.

Hakimu Lyana aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 14 mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na kuagiza mshtakiwa kurudi rumande kwa kuwa mahakama haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

# RC awahakikishia fidia waliopisha mradi ujenzi wa uwanja wa ndege

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amewahakikishia wananchi wote ambao wamepisha upanuzi wa uwanja wa ndege ulioko Ibadakuli mkoani mwake watalipwa fidia.

Alibainisha hayo juzi alipotembelea kuona maendeleo ya ujenzi wa uwanja huo na kuzungumza na baadhi ya wananchi ambao walifika kutoa malalamiko ya madai ya fidia.

Mndeme alisema kilio chao amekisikia na kuahidi kufanyia kazi mapema iwezekanavyo. Wote watalipwa fidia, lakini waendelee kuwa wavumilivu wakati mchakato wa kuwalipa ukiendelea.

Pia, aliwataka wananchi wanaoishi jirani na uwanja huo kuchangamkia fursa za ajira. Ameshatoa maelekezo kwa mkandarasi wananchi wanaoishi jirani na uwanja huo wapewe kipaumbele cha ajira ili wanufaike na mradi huo.

Vilevile, Mkuu wa Mkoa alimtaka mkandarasi kuendelea na kasi aliyonayo kujenga uwanja huo ili ukamilike ndani ya muda wa mkataba na kuanza kutoa huduma kwa wananchi kuondoa adha kufuata huduma hiyo jijini Mwanza.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Shinyanga, Mibara Ndirimbi, alisema ulipaji fidia wananchi unaendelea.

Alifafanua kuwa awali kulitokea tatizo la uthamini. Baadhi yao walilipwa fedha nyingi na wengine kidogo.

Meneja huyo alisema kuwa hicho ndicho kilisababisha wachelewe kumalizia ulipaji huo wa fidia kwa kuwa walilazimika kufanya uthamini upya kwa baadhi ya watu ambao walipunjwa malipo yao.

Alisema kuwa kwa sasa ujenzi wa uwanja huo umefikia asilimia nne na mkandarasi, kampuni ya CHICO alitia saini mkataba Aprili mwaka huu. Mradi unapaswa kukamilika Novemba mwakani ukigharimu Sh. bilioni 52.68.

Meneja Miradi kutoka Kampuni ya CHICO, Shi Yinlei, alimwaahidi Mkuu wa Mkoa kuwa ujenzi wa uwanja huo utakamilisha kwa wakati kwa mujibu wa mkataba na watajenga kwa ubora kwa kuwa vifaa vyote vya ujenzi wanavyo.

Baadhi ya wananchi wa Ibadakuli, akiwamo Charles Nkenyenge, walimwomba Mkuu wa Mkoa kuwasaidia kupata fidia zao kwa kuwa ni muda mrefu tangu wapishe mradi huo na wamekuwa wakifuatilia malipo hayo bila mafanikio. Pia waliomba kupatiwa ajira katika mradi huo.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MBAGALA | MAMU PHARMACY | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.151,KITALU 'Q10' HATI NAMBA 143195-KIBAMBA | AHMAD KASSIM OMARY | KIBAMBA | 17/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | NEZAK INVESTMENT LTD | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1019002 KIWANJA NAMBA P23439 KIFURU-KINYEREZI 2. NYUMBA YENYE HATI NA. 70437 KIWANJA NA. '213', KITALU '14' BUNJU KINONDONI | 1. ZACHARIA ANTHONY KAPAMA 2. DAFROSA ATHONY KAPAMA | 1.KIFURU KINYEREZI-ILALA 2.BUNJU KINONDONI | 15/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | WAWA COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 115345, KIWANJA NAMBA 124, KITALU '24' KIBADA KIGAMBONI 2.NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1002975 KIWANJA NA. 2483, KITALU 'A' MBEZI MANYEMA 3.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.KND/KGG/KATI/214 KIGOGO KATI 4. NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOPO | 1.SALUM JUMA NYANDOTO 2. SALUMU JUMA NYANDOTO 3.SALUM JUMA MARWA 4.SALUMU JUMA NYANDOTO | 1.KIBADA- KIGAMBONI 2.MBEZI MANYEMA 3.KIGOGO KATI 4.KINZUDI GOBA | 15/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | FRANK JACKSON KASONGA | 1. NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI TMK 046855 KIBONDE MAJI '' A'' CHARAMBE 2.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI TMK 013567MBAGALA KIBURUGWA 3.NYUMBA YENYE HATI NA.85480,KIWANJA NA.1302 KITALU 'L' MBAGALA | FRANK JACKSON KASONGA | 1.MBAGALA CHARAMBE 2.MBAGALA KIBURUGWA 3.MBAGALA RANGI TATU | 16/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MAIN | TOMONI FARMS LIMITED | SHAMBA LENYE HATI YA MAUZIANO YA SERIKALI YA KIJIJI, EKARI 194 | FRANKLIN G. BAGALLA | KIJIJI CHA TOMONI-KIBITI RUFIJI | 23/11/2023 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | LUCAS NTIRUHUNGWA MZYENGE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JAPHET YONA MZAVA | KIGAMBONI | 20/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | KOKUBELWA PAUL NGAMBEKI | KIWANJA | ANTHONY AARON ICHWEKELEZA | MPIJI MAGOE | 10/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 10/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA ZENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 11/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 11/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | MWANJELWA , MBEYA MJINI | 11/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | EMANUEL MOYO MASETA | 1.NYUMBA (3) 2.KIWANJA | EMANUEL MOYO MASETA | 1.IFWEKENYE -MBOZI 2.SONGWE | 13/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | NDIMBWELU BANDEKISYE KAFWENDA | NYUMBA | PAULO KALOTA NDAWILA | NZOVWE-MBEYA | 12/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | IPYANA TIGER JUNIOR | NYUMBA | IPYANA TIGER JUNIOR | ILEMI-MBEYA | 16/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BRAITON REBEN MWANKEMWA | NYUMBA | BRAITON REBEN MWANKEMWA | IVUMWE | 16/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | IDD SALUMU HUSSEIN | NYUMBA | EDITH JOSEPH CHIWAMILA | ISYESYE | 26/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | CHARLES JOHN ZIMBA | NYUMBA | CHARLES JOHN ZIMBA | ITEZI -MASHARIKI | 25/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | KITETE-MBEYA | 20/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | MARIAM BATON MWANDENENE | NYUMBA | VUMILIA ELIAS NYAGAWA | NGOSI- MWAKIBITI | 23/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | SONGALELI SAMA MZEE | KIWANJA | SONGALELI SAMA MZEE | BUSWELU MWANZA | 16/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | GRACE ADONIAS MTEGO | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.22 KITALU 'N' HATI NA.4870 | BLASIUS SWAI KAGINA | BUNDA | 17/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | ABAS HAMAD ISSA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI-MWANZA | 20/11/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARIA JOHN PETRO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOHN PETRO KALISA | KILOLELI 'B' - MWANZA | 21/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA 2. KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.IGELEGELE BUGARIKA 2. BUJINGWA-MWANZA | 15/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | SELEMANI CHARLES MNIKO | NYUMBA | SELEMANI CHARLES MNIKO | MBUGANI -MWANZA | 10/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | EMMANUEL LUKINDA LUTIMA | BUS TATA T847 DKN | EMMANUEL LUKINDA LUTIMA | MWANZA MJINI | 16/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JOSEPH MAKALA MAKALA | NYUMBA | JOSEPH MAKALA MAKALA | NYASAKA ILEMELA MWANZA | 20/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JAMES JACOB KALULEMA | NYUMBA | JAMES JACOB KALULEMA | MAHINA KANYERERE-MWANZA | 20/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | VICTOR STEVEN MANG'ANA | NYUMBA | VICTOR STEVEN MANG'ANA | UKONGA | 14/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | ROBERT CHACHA NYAMBARI | NYUMBA | ROBERT CHACHA NYAMBARI | KITUNDA MTAA WA KINYANTIRA | 20/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | PAULO GIRIMBE RAWE | NYUMBA | PAULO GIRIMBE RAWE | KIVULE-ILALA | 14/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | HP PLANNERS & EVENTS MANAGEMENT LTD | NYUMBA (2) | 1.JAMES NDASKOI NNKO 2.DAPHROSER ABEID HAMZA | 1.TEGETA 2.KIGAMBONI | 20/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | JOSTER JACKSON NSASHE | NYUMBA | KERAMBO CHOGO KERAMBO AND JOASTER | KITUNDA MZINGA | 16/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | MHINA JOSEPH KWELLA | NYUMBA | MHINA JOSEPH KWELLA | PUGU | 21/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KINONDONI | VAM COMPANY LIMITED | NYUMBA | VENANT ANGELO BAKEMYA | BUNJU | 09/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | OSCAR JOSSEY MUNIS | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | VERAELI ELIYA KOMBE | MWANANYAMALA -KINONDONI | 17/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | RAYSONS AND COMPANY | NYUMBA | RAYMOND MICHAEL MREMI | KIBAHA | 17/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MARIAM PATRICK SHAYO | NYUMBA | DORICE YOHANA MWAKAPESA | MBEZI MSAKUZI | 17/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | DAVID RIGHTON MINGA | NYUMBA | DAVID RIGHTON MINGA | KILUVYA | 26/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | AMINA CLEMENS NAZA | NYUMBA | ABASI ZUBERI CHANZI | KIBAMBA KIBWEGERE | 25/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | ADAM ABDALLAH ISSA | NYUMBA | ADAM ABDALLAH ISSA | MBAGALA | 20/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | ALBERTO SHEDRACK KUMWILU | NYUMBA | ALBERTO SHEDRACK KUMWILU | MBEZI LUIS | 23/11/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MLIMO COMPANY LTD | NYUMBA | TIMOTH ANISETH KATWELA | KIMARA TEMBONI | 16/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MSIBA RAYMOND MSIBA | NYUMBA | MSIBA RAYMOND MSIBA | KILUVYA | 21/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | OBEDI ZIHIRWADI MSINGA | NYUMBA | OBEDI ZIHIRWADI MSINGA | KIBAHA KWA MATHIAS | 28/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | NORBERT LUDOVICK KWIYAKA | NYUMBA | NORBERT LUDOVICK KWIYAKA | CHAMAZI DOVYA | 20/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | MTUMWA SALUM HAMAD | NYUMBA | MATONGO NKWABI NSWAGA | KIGOGO | 21/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | AMANI OMARI NOMBWANI | NYUMBA | AMANI OMARI NOMBWANI | KIGOGO-KIGAMBONI | 15/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | MAIMUNA ISAYA KIRINDO | NYUMBA | MAIMUNA ISAYA KIRINDO | MJI MPYA | 28/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | PADONI KIBAYU SIMON | NYUMBA | PADONI KIBAYU SIMON | MAJOHE | 23/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | LISTER BENEDICT CHIMYA | NYUMBA | LISTER BENEDICT CHIMYA | KIMARA | 28/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | ATUPELE LABAN MWAIJIBE | NYUMBA | ATUPELE LABAN MWAIJIBE | KIPUNGUNI-KIPAWA ILALA | 30/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | HAMISI MESHACK NGINYANYI | NYUMBA | HAMISI MESHACK NGINYANYI | TABATA-LIWITI | 30/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | ALLY SHAWEJI OMARY | NYUMBA | ALLY SHAWEJI OMARY | KIBAMBA | 28/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | SALUM RAJABU MCHOMVU | NYUMBA | SALUM RAJABU MCHOMVU | KICHANGANI- MAJOHE | 21/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | EDNA ISHENGOMA RWEMILINZI | NYUMBA | EDNA ISHENGOMA RWEMILINZI | TEGETA 'A' | 7/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | HAMZA KASSIM NGOMANGO | NYUMBA | HAMZA KASSIM NGOMANGO | CHANIKA ZINGIZIWA | 23/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | NAHALI ALLY LIPWAI | NYUMBA | NAHALI ALLY LIPWAI | KIBAHA KONGOWE | 5/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | AMINA MUSTAFA SHIRAHE | NYUMBA | AMINA MUSTAFA SHIRAHE | KINYEREZI | 5/12/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | YOVANALI SAIMONI MAGIGE | NYUMBA | YOVANALI SAIMONI MAGIGE | GONGO LA MBOTO | 23/11/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0715868000/0714939933/0785242219/0759282344**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

# Wauguzi wadaiwa kuomba rushwa wajawazito

**Na Halima Ikunji,** TABORA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Tabora imesema inaendelea na uchunguzi kuhusu taarifa za baadhi ya watumishi wa idara ya afya kuomba rushwa kwa wajawazito.

Zaidi ya watumishi 20 wa kada hiyo wanadaiwa kuomba rushwa kwa wajawazito. Pia wamo wanaodaiwa kutoa lugha chafu kwa wagonjwa wanaofika vituoni kupatiwa huduma.

Juzi Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Tabora, Musa Chaulo alibainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu taarifa ya utekelezaji wa shughuli zao kwa miezi mitatu.

Alisema wamepokea taarifa za tuhuma hizo kwamba baadhi ya watoa huduma katika vituo vya afya na zahanati za wilaya mbili ambazo hakuzitaja, wanajihusisha na vitendo hivyo ambavyo ni kinyume cha maadili ya kazi.

"Wauguzi hao wamekuwa wanaomba rushwa kinamama wajawazito wanapofika katika vituo vyao kwa ajili ya kujifungua, jambo ambalo ni kinyume cha taratibu za Wizara ya Afya na wakati mwingine kuwakosesha huduma stahiki wahitaji hao," alisema.

Chaulo alisema taasisi hiyo inaendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kupiga vita vitendo vya rushwa. Pia wanashirikiana na Jeshi la Polisi kufuatilia kwa kina vitendo hivyo.

Hata hivyo, kiongozi huyo wa TAKUKURU alisema wanafanya uchunguzi dhidi ya askari polisi wanaotuhumiwa kuomba rushwa ili kutoa dhamana kwa watuhumiwa wa makosa mbalimbali.

Alisma tayari taasisi hiyo imechukua hatua dhidi ya askari aliyedaiwa kujihusisha na utovu wa nidhamu. Wamefungua kesi ya jinai dhidi yake. Inaendelea mahakamani.

Alisema TAKUKURU inaendelea kutoa elimu ya kuzuia na kupambana na rushwa kwa makundi mbalimbali ya kijamii ili kuwapa fursa ya kutoa taarifa wanapobaini vitendo vya namna hiyo katika maeneo yao.

Chaulo pia alisema wanaendelea kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji miradi ya maendeleo na kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu.



Mhandisi Aron Mwaiganga wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi, akitoa ufafanuzi kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Mhandisi Cyprian Luhemeja (kulia), kuhusu maendeleo ya ujenzi wa kiwanda hicho mkoani Morogoro, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Mifuko hifadhi ya jamii iwekeze kuchochea uchumi, fursa za ajira'

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Cyprian Luhemeja ameitaka mifuko ya hifadhi ya jamii kuendelea kuwekeza katika miradi ya uzalishaji ili kuchochea uchumi na fursa za ajira nchini.

Baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi mkoani Morogoro jana, Luhemeja alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa kibali na kuridhia ujenzi huo.

Alisema uwekezaji wa aina hiyo una faida kubwa kiuchumi. Mradi huo unatarajia kutoa ajira zaidi ya 10,000 kwa Watanzania.

"Uwekezaji wa miradi ya uzalishaji kama huu wa kiwanda cha Mkulazi unaongeza ajira na kukuza uchumi. Kukamilika kwake pia kutasaidia kupunguza changamoto ya upungufu wa sukari nchini na kuondoa uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni Hodhi ya Mkulazi, Dk. Hildelitha Msita, aliahidi bodi yake itatekeleza maelekezo aliyotoa Katibu Mkuu Luhemeja ikiwamo mpango wa kuongeza eneo la mashamba kwa ajili ya kilimo cha miwa.

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, alisema NSSF itaendelea kutoa ushirikiano kwa Mkulazi ili kuhakikisha kiwanda hicho kinaanza uzalishaji.

Mwakilishi wa Shirika la Uzalishaji Mali (SHIMA), Muyengi Bulilo, aahidi kuendelea kuhakikisha ulinzi na usalama kwenye eneo hilo.

Awali akitoa taarifa kuhusu maendeleo ya mradi huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni Hodhi ya Mkulazi, Selestine Some alisema kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha tani 75,000 za sukari kwa mwaka na kinatarajiwa kuanza na uzalishaji wa tani 50,000 za sukari.

## Uhaba wa watumishi sekta ya ujenzi wapatiwa dawa

**Na Frank Monyo**

KUKABILIANA na uhaba wa watumishi katika sekta ya ujenzi, Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS), Mohamed Besta amefungua mafunzo ya siku 10 ya wahandisi wapya 49 walioajiriwa na serikali.

Wahandisi hao watapelekwa kufanya kazi maeneo mbalimbali nchini ili kupunguza uhaba wa watumishi wa kada hiyo.

Baada ya kufungua mafunzo hayo Dar es Salaam juzi, Besta alisema huo ni mwendelezo wa hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali kuwawezesha kitaaluma wahandisi ili wasimamie vizuri kazi za ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja.

"Mafunzo haya yamefanyika kuwaongeza chachu na kupata wahandisi wapya wenye uelewa. Lengo ni kuimarisha utendaji kazi hasa katika usimamizi wa viwango katika ujenzi wa barabara.

"Hivyo, ninachukua fursa hii kumshukuru Rais wetu, Wizara ya Ujenzi na serikali kwa ujumla kwa kutoa kibali kwa TANROADS kuajiri wahandisi wapya kabisa ambao watakwenda kuongeza ufanisi hasa katika maeneo ambayo wahandisi wametoka kwa kustaafu ama kuhamia maeneo mengine.

"Lazima tuwajenge wahandishi wapya. Ninawataka wafahamu kwamba wanakwenda kuhudumia miundombinu ya takribani Km 36,760 nchi nzima pamoja na miradi mingi inayoongezeka si katika ngazi ya kitaifa tu, bali pia kwa ngazi ya mikoa.

"Tutaendelea kuwasimamia na kutoa mafunzo ya namna hii mara kwa mara ili kuendelea kuwajengea uwezo kwa jinsi ambavyo teknolojia inavyoendelea kubadilika," alisema.

Meneja Rasilimali Watu na Utawala wa TANROADS, Pilika Kasanda, alisema watumishi hao wapya ambao wameajiriwa kuanzia mwezi uliopita ni mwendelezo wa utekelezaji wa maelekezo ya serikali ya kuajiri jumla ya watumishi 125 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hususani miradi mipya ambayo inaendelea kutekelezwa na serikali ikiwamo ya EPC + F.

"Serikali imetoa kibali waajiriwe wahandisi 63 na mafundi 62, jumla 125. Katika kibali hicho awamu ya kwanza tumepata wahandisi 49 ambao wameanza kufanyiwa taratibu za awali za ajira, tulianza na mafunzo ya utayari wa kuajiriwa kwenye utumishi wa umma na leo tumeendelea na mafunzo ya kitaaluma ambayo yametolewa na wakufunzi wetu wa ndani.

"Lengo ni kuwawezesha na kuwajengea uwezo wahandisi hawa wapya kabla ya kwenda kufanya kazi kwenye maeneo mbalimbali ya mikoa ya Tanzania Bara," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Utafiti na Maendeleo kutoka Maabara Kuu ya Utafiti wa TANROADS, Mussa Mataka alisema mafunzo hayo yatajumuisha maeneo yote makuu ya ujenzi wa barabara.

## Waziri: NCAA isimamie haki zote za watumishi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki, ameitaka menejimenti ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) kusimamia kwa ukamilifu haki zote za watumishi wa mamlaka hiyo ili kuboresha utendaji.

Angellah alielekeza kuangaliwa upya kwa haki hizo jana alipokuwa Wilaya ya Karatu, mkoani Arusha, baada ya kusikiliza hoja mbalimbali za watumishi hao.

Kwa mujibu wa Kairuki, watumishi wanapofanya kazi katika mazingira mazuri, huinua tija katika mamlaka na hivyo kuimarisha uchumi wa taifa.

"Mafanikio mliyoyapata kwa mwaka wa fedha 2022/23 ya kuongeza idadi ya watalii kutoka 425,386 mpaka 752,512, yanatokana na kuwa na watumishi wanaojituma na kuthamini kazi zao, hivyo ni vyema mkaendelea na utaratibu huohuo wa kusimamia maslahi na haki zao za msingi," aliagiza.

Waziri huyo pia alisema kwa kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii ni tegemeo kubwa katika uchumi wa taifa, ni vizuri kila mtumishi akatambua wajibu wake na kufanya kazi kwa kujituma, ubunifu, uaminifu na weledi wa kutosha ili kuchangia kuongeza mapato yanayotokana na sekta hiyo.

Vilevile, Waziri Angellah alisisitiza kwamba hayuko tayari kumtetea mtumishi yeyote mzembe, mlarushwa na asiyefuata taratibu za kiutumishi katika utendaji wake wa kazi kwa kuwa siku zote haki inakwenda pamoja na wajibu.

"Huko nyuma nimekuwa mbunge kwa miaka 10 kupitia vyama vya wafanyakazi, hivyo sitaki kuona mtumishi akinyanyaswa, jengeni utaratibu wa kusimamia haki za kila mtumishi na wapeni nafasi ya kufanya kazi kwani hakuna mtumishi mbaya kama atasimamiwa vizuri na kuelekezwa," alisema.

Katika kikao hicho watumishi kutoka idara mbalimbali walipata fursa ya kueleza njia mbalimbali za kuimarisha sekta ya utalii na changamoto wanazokabiliana nazo katika utendaji wao wa kazi za kila siku.

Baadhi ya dosari walizoomba zifanyiwe kazi ni miundombinu ya kuingia katika hifadhi hasa ujenzi wa barabara zinazopitika muda wote, kuwe na majengo bora ya kutolea huduma na kupata stahiki zao kwa wakati ili wafanye kazi kwa tija.

Waziri huyo aliahidi kufuatilia kwa karibu changamoto hizo na kuhakikisha kuwa zinapatiwa ufumbuzi huku akisisitiza umuhimu wa kila mtumishi kujituma na kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma.

# RC acharuka wafanyabiashara vileo kususa kikao cha serikali

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAFANYABIASHARA wanaozalisha na kuuza vileo mkoani Kilimanjaro, wamemchefua Mkuu wa Mkoa huo, Nurdin Babu baada ya kususia kikao kilichoitishwa na serikali kwa lengo la kujadili mambo mbalimbali.

Kutokana na hali hiyo, Babu ameonya wafanyabiashara hao, akiwataka kuacha utamaduni wa kuuza malighafi nje ya nchi badala yake waanzishe viwanda vya kuongeza thamani mazao yanayozalishwa.

Mkuu wa Mkoa alieleza masikitiko yake jana alipozungumza na wajumbe wa Baraza la Wafanyabiashara Mkoa wa Kilimanjaro kuhusu alivyoumizwa na kitendo hicho.

"Juzi hapa tuliita kikao cha wafanyabiashara wa vileo hapa mkoani baada ya kupokea kero mbalimbali juu ya upigaji wa muziki kupita viwango vinavyotakiwa kwa mujibu wa sheria.

"Tumewaita wamekataa kuja, hili hatutalivumilia likijitokeza tena. Ninapowaita njooni tuzungumze, tujadiliane, tutafikia tu mwafaka," alisema Babu.

Mkuu wa Mkoa alisisitiza kuwapo kwa ushirikiano na kukubali wito ni moja ya mambo yanayotoa fursa pana ya kutatua matatizo mbalimbali ya wafanyabiashara.

"Kama kuna upungufu ni vizuri tukaitana, tukaonyana, tukashauriana kama kuna sheria kandamizi zinazochangia kutofanya biashara vyema, tuziandikie na zifanyiwe marekebisho. Hiyo ndiyo maana halisi ya sisi viongozi kuwapo hapa," alisema.

Babu pia aliwataka wafanyabiashara hao kuridhika kufanya biashara katika maeneo wanayopangiwa na halmashauri zao ili wawekewe miundombinu sahihi itakayowawezesha kufanya biashara katika mazingira bora zaidi.

"Wapo wafanyabiashara ambao wamekuwa wakaidi, nyakati za jioni wanapanga bidhaa zao katika maeneo mbalimbali ya ofisi za serikali na barabarani.

"Hili hatutalikubali, waambieni wabadilike, tumieni taasisi za fedha kukopa ili kuboresha biashara zenu," alisema Babu.

Awali Katibu Tawala wa Mkoa huo, Tixon Nzunda, alielekeza wakurugenzi wa halmashauri za wilaya zote na manispaa kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya wafanyashara wadogo ikiwa ni pamoja na kuwapa elimu kupitia wataalamu ili kuleta tija kwenye biashara zao.

Katika kikao hicho, baadhi ya wafanyanyabiasha wanaopanga bidhaa zao pembezoni mwa barabara katika Manispaa ya Moshi, akiwamo Winifrida Lawrence, walisema wamekuwa wanafanya biashara hizo katika maeneo hayo kutokana na maeneo waliyopewa kutokuwa na mwingiliano mkubwa wa watu.

"Hatupendi kufanya biashara katika maeneo kama haya, lakini tunalazimika kwa kuwa tunafanya biashara ndogo ambazo watu wanazihitaji hasa nyakati za jioni, na watu hao hupatikana maeneo hayo. Serikali iangalie upya namna hiyo ya kutupanga," alisema Faustina Maro.



Mkurugenzi wa Idara ya Wanawake ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Juliana Kibonde (wapili kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mwakilishi wa Jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi wilaya ya Rombo linalowezeshwa na asasi ya AJISO, Maria Kimongi (wa pili kulia), kuhusu masuala mbalimbali ya jukwaa hilo, wakati wa uzinduzi wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake mkoa wa Kilimanjaro, mjini Moshi hivi karibuni. **PICHA: JAMES LANKA**

# Wenyeviti wa vijiji waonywa kugeuza mtaji migogoro ardhi

**Na Dege Masoli,** KILINDI

SERIKALI imenyooshea kidole na kuonya wenyeviti wa vijiji katika Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga waliogeuza migogoro ya ardhi kuwa mitaji yao ya kiuchumi kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwakani.

Jana Mkuu wa Wilaya ya Kilindi, Hashim Mgandilwa, alisema mbali na kuifanya migogoro hiyo kuwa sehemu ya kujiingizia kipato, pia wanaitumia kama mtaji wa kisiasa kuelekea uchaguzi huo.

Mgandilwa alitoa angalizo hilo wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo alipopewa nafasi ya kutoa salamu za serikali.

Alisema vyanzo vya migogoro ya ardhi na mipaka ya kiutawala wilayani mwake kwa asilimia kubwa ni viongozi hao ambao huitumia kama miradi ya kujipatia fedha na nguvu za kisiasa.

"Kiongozi ambaye migogoro ya ardhi kwake ni mradi wa kupata fedha, njia ya kuutatua ni kumtatua yeye kwanza vinginevyo migogoro hiyo haitaisha katika eneo hilo. Ninawaonya wenye tabia hiyo acheni mara moja," alisisitiza Mgandilwa.

Kuhusu migogoro ya mipaka ya vijiji, Mkuu wa Wilaya alielekeza idara husika kufuata taratibu za utatuzi wake, ikiwamo kanuni za upimaji ardhi za mwaka 1974/1975 na 1994/1995 na ile ya mwaka 2007/2008, ambayo mchakato wake unaanzia ngazi ya kijiji na kata kabla ya kwenda hatua za juu.

"Sasa kilichotokea ni changamoto za presha za uchaguzi ambazo zilisababisha baadhi ya vijiji kuanzisha pasipo kufuata taratibu, kanuni na sheria za upimaji na ndiyo matokeo ya migogoro hii inayotusumbua sasa," alisema Mgandilwa.

Aliwataka madiwani na wenyeviti wa vijiji kusimamia kanuni, taratibu na sheria kwenye maeneo yao ili kuondoa migogoro ya ardhi isiyoisha kwa kuwa imo katika uwezo wao.

Akitoa ufafanuzi kuhusu migogoro hiyo, Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Tanga, Tumaini Gwakisa, aliwaonya wataalamu wa ardhi na maofisa ardhi wateule ngazi ya wilaya kuacha kulea migogoro hiyo huku akiwataka kuzingatia maadili ya kazi zao badala ya kuwa sehemu ya vyanzo vya migogoro.





HOJA YA CAG BADO GIZANI...

# Ijue shule yenye vyoo vilivyotitia na hatari afya ya wanafunzi 950

## ●Miaka 3 watoto wahamia vichakani; wahusika wakiri, ila bajeti ya ukombozi nayo tata...



Muonekano wa choo kilichokuwa kikitumiwa na wanafunzi kilichoharibika kwa kutitia na kuzuiliwa kutumika kabisa. Shule hiyo ina matundu ya vyoo sita pekee hali inayowalazimu wanafunzi kutumia matundu matatu kwa kila jinsia. **PICHA: ALEX SAYI**

**Na Alex Sayi,** MASWA

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Isulilo, Kata ya Busangi wilayani Maswa mkoani Simiyu wako hatarini kukumbwa na magonjwa ya mlipuko kutokana na uhaba wa matundu ya vyoo shuleni huko.

Inaelezwa kuwa, ni zaidi ya miaka mitatu sasa tangu kutitia kwa vyoo vilivyokuwa vinatumika. Havijafanyiwa marekebisho wala kujengwa vingine vipya.

Kwa nyakati tofauti baadhi ya wanafunzi na wahitimu wa shule hiyo walieleza kuwa ukosefu wa huduma hiyo imekuwa kero na adha kubwa kwa wanafunzi.

Abel Mwandu, mwanafunzi wa darasa la nne shuleni huko, alimwambia mwandishi kuwa kwa muda mrefu hali hiyo imekuwa inawalazimu kwenda kujisaidia vichakani na kuhatarisha afya zao.

"Nilikuwa darasa la tano wakati vyoo vinatitia, hadi nimehitimu hakuna vyoo vipya vilivyojengwa. Tulikuwa tunajisaidia vichakani tu na sasa hivi wanajisaidia vichakani maana matundu yaliyoko hayatoshelezi na wakati wa mapumziko tulikuwa tunalazimika kupanga foleni kusubiri huduma hiyo," alidai Lukas Abel, mhitimu wa darasa la saba mwaka huu.

Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inaelekeza: "Wananchi watashiriki shughuli za serikali yao kwa mujibu wa Katiba hii".

Katika hilo, Bushile Ng'wandu, mzazi na mkazi wa Kijiji hicho, alimwambia mwandishi kuwa wamekuwa wakiwashuhudia wanafunzi hao wanavyosumbuka na kueleza kuwa licha ya kukakaa vikao kujadili utatuzi wa kero hiyo, uongozi umeendelea kuwa kimya kushughulikia shida hiyo.

Mboje Njile, mzazi na mkazi wa kijiji hicho alisema kuwa kufuatia adha hiyo walilazimika kuchangishana na baadhi ya wadau wa maendeleo ili kufyatua matofali kwa ajili ya ujenzi wa boma la vyoo, lakini wakaishia kufyatua matofali 600. Ni kutokana na Ofisa Mtendaji wa Kiiji kuwataka wasitishe kazi hiyo.

"Mtendaji alisema kuwa diwani anafuatilia suala hilo halmashauri, lakini ni muda sasa hatujaona kinachoendelea," alidai Njile.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Madame Ndalahwa alithibitisha kuwapo adha hiyo na kueleza kuwa hadi sasa hakuna ujenzi wa vyoo uliofanyika licha ya shule hiyo kuwa na wanafunzi zaidi ya 950.

"Ni kweli tatizo ni kubwa na hakuna maboresho yoyote yanayoendelea hadi sasa. Matundu yaliyopo hayatoshi kulinganishwa na idadi ya wanafunzi zaidi 950 waliopo shuleni hapa kwa sasa," alisema Mwalimu Ndalahwa.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Marko Malimi alisema michango ya wananchi na wadau wa maendeleo waliyochangia ilisaidia kunyanyua boma lililofikia hatua aliyoita nzuri.

Alisema hatua iliyobaki, Malimi alisema aliahidiwa na diwani kuwa anafuatilia suala hilo halmashauri. Ndiyo sababu ya kusitisha uchangishaji fedha kwa wananchi.

Diwani Paulo Nyondwa alieleza kuwa anaendelea kulifuatilia suala hilo halmashauri ili wanafunzi hao wasome katika mazingira salama.

Ofisa Elimu Taaluma Halmashauri ya Maswa, Neema Makundi, alisema halmashauri inaendelea na mpango wa uboreshaji huduma ya vyoo kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

Makundi aliongeza kuwa idara ya elimu na halmashauri wanatambua ukubwa wa tatizo kwa wilaya yote na wanaendelea kulitafutia utatuzi kadri fedha zinavyopatikana.

"Tayari tumeshapokea Sh. bilioni 1.6 za P4R (Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo) na Sh. milioni 331.8 toka Serikali Kuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya elimu," alisema.

Ofisa Elimu huyo alibainisha kuwa Shule ya Msingi Isulilo imetengewa Sh. milioni 30 kwa ajili ya matundu 14 vyoo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Mwongozo wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wa ujenzi wa miundombinu shuleni, unaelekeza tundu moja la choo lijengwe kwa gharama ya Sh. milioni 1.1.

Kwa mujibu wa uwiano uliopo kati ya fedha zilizotolewa na mwongozo, ina maana Sh. milioni 30 zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa matundu 14 ya vyoo shuleni Isulilo zinazidi uhalisia. Hii ina maana kwamba kila tundu la choo litajengwa kwa Sh. 2,142,857.14 (milioni 2.143/-).

Ofisa Elimu alisema: "Kama nilivyosema awali, uhitaji wa matundu ya vyoo kwa wilaya ni mkubwa na tumeshapokea fedha za P4R Sh. bilioni 1.6 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, vyoo na nyumba za watumishi na Sh. milioni 331.8 toka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo kwa shule za msingi 12 ikiwamo hiyo ya Isulilo."

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 inaelekeza uwiano wa vyoo na wanafunzi shuleni uwe tundu moja kwa wavulana 25 na tundu moja kwa wasichana 20, hivyo kwa kurejea idadi ya wanafunzi 950 waliopo shuleni Isulilo, kunahitajika wastani wa matundu 38 kukidhi mahitaji hayo ya kiafya shuleni.

Maisha Mtipa, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, alimwambia mwandishi kuwa halmashauri inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya uboreshaji huduma ya vyoo katika shule za msingi zote wilayani mwake ili kunusuru adha iliyopo sasa.

"Kwa kweli shule nyingi zinakabiliwa na changamoto hii na mimi nilishafika Shule ya Msingi Isulilo nikiwa na diwani kujionea hali ilivyo.


"Kama halmashauri tumeshatenga fedha kwa ajili ya shule hii Sh. milioni 30 ili kuboresha huduma ya vyoo shuleni huko," alisema Mtipa.

Kimsingi, kinachoshuhudiwa shuleni Isulilo si tu kwamba kinakinzana na maelekezo ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, bali pia ni ishara ya kutotelekezwa hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2017.

Mnano Machi 2017, CAG (kipindi hicho Prof. Mussa Assad) alitoa Ripoti ya Ukaguzi Maalum wa Miundombinu na Samani za Shule za Msingi Tanzania, akibaini kuwa shule nyingi zinazomilikiwa na serikali zilikuwa na hali mbaya kimiundombinu na Samani.

CAG Assad alipendekeza serikali ifanye ukarabati wa samani na miundombinu iliyopo na kujenga mipya ili kuimarisha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji nchini.

**Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Madame Ndalahwa alithibitisha kuwapo adha hiyo na kueleza kuwa hadi sasa hakuna ujenzi wa vyoo uliofanyika licha ya shule hiyo kuwa na wanafunzi zaidi ya 950.**




Ukurasa 13

Siku ya Nyerere itazamwe upya

BUFE
IJUMAA NOVEMBA 3, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



KANUNI ZAKE HIZI... ZAIDI YA PESA... Mtaalamu afunguka uchochoro wa mjasiriamali kufika ngazi mafanikio

Ukurasa 12

## MGENI RAIS UJERUMANI KWA SAMIA...

# Diplomasia Uchumi kwenye sekta ya Utalii, wakikamilisha yaliyokwishaanza kwa hatua

• Alishafika nchini akiwa waziri, wabia wa Mlima Kilimanjaro


**Na Peter Orwa**

MWANZONI mwa wiki hii, Rais Samia Suluhu Hassan nchini, alipata ugeni wa Rais Frank- Walter Steimeier wa Ujerumani, katika ziara ya siku tatu, ambako kwa kuanza akawa na mazungumzo na baada ya hapo akawaambia wanahabari:

"Nimekuwa na mazungumzo na Rais wa Shirikisho la Ujerumani Frank Walter Steinmeier, ambaye yuko nchini kwa ziara ya siku tatu ya uhusiano wa kidiplomasia wa siku tatu, kati ya nchi yetu na Ujerumani umedumu kwa zaidi ya miaka sitini," anatamka Dk. Samia akiwa na mwendelezo: "Ujerumani ni mbia wetu muhimu katika biashara na sekta mbalimbali za maendeleo, ikiwamo maji, afya na mazingira."

Katika tafsiri pana, ugeni wa Rais wa Ujerumani unatajwa kutoa heshima kubwa kimataifa katika diplomasia ya Tanzania, msingi wake ukijikita barani Afrika, akizuru pia nchini Zambia, ambako Rais Dk. Samia alikuwa huko karibuni. Hilo linafanyika, huku Kansela Angela Merkel, naye katika tarehe hizo alikuwa nchini Nigeria, kisha akasonga kwa majirani Ghana kuwekeza katika diplomasia uchumi.

Ikirejewa miezi kadhaa iliyopita, Kansela Merkel baada ya kuanza kwa vita vya Russia na Ukraine, Ujerumani ikitegemea nishati ya Russia, ikatangaza kubadili mwelekeo kuanza kununua katika vyanzo vingine barani Afrika. Muda mfupi ikasikika Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, akienda kuingia makubaliano ya awali kununua nishati nchini humo.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa na mgeni wake, Rais wa Shirikisho la Ujerumani Frank Walter Steinmeier. **PICHA: MAKTABA.**

Ndiyo katika sura hiyo, Rais Steimeier wa Ujerumani amekuwa katika mtazamo huo. Huku akiwa mwenyeji nchini maana wakati akiwa Waziri wa Mambo ya Nje, alishawahi kuzuru nchini. Ni aina ya simulizi na matendo yanayoakisi hatua za miaka miwili ya utawala wa Rais Dk. Samia, akifungua milango ya Diplomasia Uchumi nchini kimataifa.

Hadi sasa moja ya maeneo,katika mawanda ya biashara na uchumi, ambayo yana mnyororo mrefu katika diplomasia ya uchumi, ni sekta ya Utalii, ambayo raia wa Ujerumani kwa mujibu wa taarifa za watalii nchini kati ya Septemba ya mwaka jana na mwaka huu, walishika nafasi ya tatu kwa wingi kuzuru nchini, jumla yao 68,796 wakishika nafasi ya tatu wakitanguliwa na Marekani na kisha Wafaransa. Wanaofuata nafasi ya nne ni Waingereza, Italia, Wahindi, Wachina, wanaotoka Poland, Uholanzi na kutoka Uhispania.

Kwa mujibu wa Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani, Dk. Benson Bana, ziara ya Rais Steimeier nchini Tanzania, ni mwendelezo wa tafsiri ya muda mrefu katika uhusiano, akitoa mfano wa sasa kumesajiliwa miradi zaidi ya 200 Tanzania Bara kutoka Ujerumani, huku Zanzibar zikiwapo zaidi ya 15, hivyo mkuu huyo wa taifa hilo la Ulaya, anaendelea kupanua wigo wa ushirikiano katika diplomasia uchumi katika milango hiyo miwili kitaifa.

Vilevile, sura ya ushirikiano ambayo inatawala kwenye historia yenye mzizi wa Vita vya Majimaji, hata Rais Steimeier katika sehemu ya ziara yake, alianza na Idara ya Makumbusho ya Taifa, kisha akatembelea mkoani Ruvuma kwenye mzizi wa historia hiyo, akisihi ni nafasi nzuri ya ushirikiano kihistoria kuchukua nafasi, ilhali Ujerumani ikiiweka fursa ya kurejesha mafuvu ya marehemu wa historia hiyo, waliofia Ujerumani.

Hata Shule ya Ualimu Dar es Salaam (DUCE), ambayo ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ni zao la msaada wa Ujerumani, katika miaka michache baada ya uhuru, wakati huo ikiitwa Chuo cha Ualimu Chang'ombe.

**UJERUMANI NA TANZANIA**

Simulizi ya namna Ujerumani inahusiana na Tanzania, ina mengi kihistoria kama anavyogusa Rais Dk. Samia, hata hivyo ikionekana kunakishiwa nako katika namna yake katika Utawala Awamu ya Sita, eneo la Diplomasia Uchumi, likigusa zaidi Utalii na Maliasili, ambako Ujerumani imekuwa ikitoa misaada lukuki, hivyo hata ziara ya Rais wa Ujerumani ni mwendelezo wa uhusiano huo.

Inaendelea Uk 12

## BIASHARA

KANUNI ZAKE HIZI… ZAIDI YA PESA…

# Mtaalamu afunguka uchochoro wa mjasiriamali kufika ngazi mafanikio

**Na Beatrice Philemon**

ILI kuanzisha biashara au mradi wenye faida na mafanikio makubwa, inatakiwa mjasiriamali au mfanyabiashara afahamu kanuni za kufanya biashara hiyo au mradi kuhudumiwa ipasavyo.

Hapo, Mkufunzi kutoka kampuni ya Madeo Finance, anaeleza kanuni zinazoweza kusaidia wafanyabiashara wadogo, kati na wakubwa kukuza biashara zao, kupata masoko mengi ndani na nje ya nchi, pia kutoa ajira inayochangia pato la taifa.

Wafanyabiashara wengi wanatajwa kushindwa kudumu katika biashara zao, kwa sababu ya kutofahamu kanuni za uendeshaji biashara, wengi wanafanya biashara kwa mazoea.

NI hatua ambayo mtaaluma huyo wa biashara, anafafanua ni shinikizo kwao lililowafanya kuona changamoto ya kubuni mradi maalumu wa kutoa mafunzo ya uendeshaji biashara kwa wajasiriamali wadogo na kati, waweze kuzalisha bidhaa zenye ubora au kutoa huduma bora zinazokidhi mahitaji ya wateja.



Shughuli za ujasiriamali zikiendelea, Kariakoo Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA.**

Pia, wanatoa mikopo midogo na mafunzo ya utunzaji kumbukumbu za biashara zao, hapo Mkufunzi Kilasi anaiambia Nipashe kwamba: "Mimi kama mkufunzi, nina furaha sana kuona hivi sasa katika maeneo ambayo nimetoa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo na kati."

"Wengi wamebadilika, wanaendesha biashara zao kwa kufuata kanuni za uendeshaji biashara na sasa hivi wanaweza kuchukua mikopo midogo midogo katika kampuni yetu," anasema.

**MAANA YA UJASIRIAMALI**

Mkufunzi Kilasi anamtaja ni mtu anayegundua au kuboresha wazo la biashara au fursa, na ili kuanzishwa biashara au mradi wenye mafanikio, lazima kuwapo ufahamu wa kanuni za kukifanya kitu hicho jinsi ipasavyo.

Anaufafanua ujasiriamali, ni zaidi ya kupata pesa, ni lazima kwanza kutatua changamoto za watu au mtu, ndipo ataweza kupata pesa kutoka kwa mtu husika au wateja wake.

Kilasi anaifafanulia Nipashe kwamba, mjasiriamali anatakiwa ajikite kwenye kutatua matatizo ya watu, akiangalia changamoto katika eneo unaloishi, pia kuna changamoto gani na anakuwa na maono ya biashara au mradi wake.

"Mjasiliamali bila kuwa na maono ni sawa na kuendesha gari isiyokuwa na usukani. Maono katika biashara yatakuwezesha kukuongoza ufanye nini na kwa muda gani," anatamka.

Pia, anataja wakati wa kuanzisha biashara au mradi wake, mjasiriamali ni lazima ajiulize kuhusu mtu nafsi yake, anataka kuwa nani, lengo Analonuia kufika baadaye.

Hilo linatajwa kuendana na bidii ya kufikia lengo husika, kwa sababu wajasiriamali waliofanikiwa ni wale walioweza kubadili maono yao kuwa uhalisia.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

Kwa mujibu wa Kilasi, mjasiriamali anatajwa kuwa na mpango mahsusi wa kibiashara, anakishika kitu kwa uimara, pasipo kubadilisha sababu za msingi, akiwa na maono ya mbali.

"Lazima uwe na kitu au biashara moja ambayo una maono nayo, pia chagua watu wa kushirikiana nao, kwa mfano mfanyakazi utakayemchagua awe na uwezo wa kufanya kazi, usichukue tu eti huyu ni rafiki au mtoto wa dada, chukua mtu ambaye yupo tayari kufanya kazi na wewe kwa moyo," anasema

Pia, Kilasi anataja umuhimu wa kuwa makini wakati wa kuchagua washiriki au watu wa kufanya nao kazi katika biashara yako au mradi ili kuhakikisha maono yako hayakwamishwi.

"Kamwe usichague mtu tu kwa kigezo kuwa ni rafiki au ndugu yako, bali chukua mtu ambaye unaamini anaweza kufanya kitu chochote kwa ajili ya kufanikisha kama mjasiliamali," anasema.

Pia, anataja biashara kufanyika kwa namna tofauti, iwe ikiboreshwa kila siku, hata bidhaa zake kufanya vizuri vizuri na anatakiwa kukumbuka uhalisia uwe ushindani mkubwa sokoni, hivyo inazaa jukumu la jitahidi za kuongeza tija, ubora wa huduma na bidhaa zako.

"Hivi leo sokoni kuna bidhaa na huduma nyingi ambazo ni za aina moja, lakini siyo zote zinafanya vizuri. Hii inatokana na baadhi ya bidhaa au huduma kutozingatia kuwa ni tija kwa wateja wake," anasema.

Lingine analolipa umuhimu ni namna ya kutumia pesa vyema, kwa mpangilio, kuchuja vitu vya kutumia ili mtaji ukue, kwani wengi wanakabiliwa na changamoto ya matumizi ya pesa, kuanzia kwenye yao binafsi.

"Ukiwa wewe ni mjasiriamali, jitahidi kufahamu wateja wako na kuwajali, fahamu wateja wako wanataka nini, sikiliza maoni na ushauri wao, hakikisha unakamilisha mahitaji yao,' anatamka na kuendelea:

"Tumia lugha nzuri na rafiki kwa wateja, mfanye mteja aone unamthamini na unatanguliza huduma kabla ya pesa."

Hadhari nyingine anayoitoa, ni kwamba mjasiriamali anapaswa kufuta mawazo kuwa wateja wanamfuata, kwani kwa uhalisia, yeye ndiye anayewahitaji kukuza biashara au huduma anayoitoa, akiwajali zaidi wateja.

Lingine katika orodha hiyo ya masomo, ni namna mjasiriamali anawajibika kujifunza kutumia tekinolojia, akitumia mitandao ili kupata wateja, kadri teknolojia inavyokua, naye apanuke kuitumia.

"Sasa tunaishi kwenye ulimwengu wa sayansi na teknolojia, kama vile simu na mtandao wa intaneti, ukitumia njia hizi unaweza kuwafikia watu wengi zaidi na kuongeza mauzo ya huduma au bidhaa yako unayozalisha," anasema, ikiendana na ukaribu kwa wateja wake.

**UKANDA WA SOKO**

Mtaalamu Kilasi, anashauri kwamba, wajasiriamali kufuata kanuni kadhaa, akiorodesha: 'Kwanza, kabisa mjasiriamali anatakiwa alifahamu soko vyema. Hakikisha huduma au bidhaa unayoitoa inakidhi mahitaji ya mteja na inafika kwenye soko stahiki.

"Kwa mfano ukiwa wewe ni mzalishaji wa mayai lakini eneo ulilopo soko ni duni, basi tafuta eneo lingine ambalo soko la bidhaa hii ni nzuri. Kwa kufanya hivi, utaweza kulenga soko na kujiongezea faida wewe kama mjasiriamali."

Pia, anarejea wajibu mkuu wa kukumbuka kanuni, sambamba na kutokata tamaa, akitumia changamoto kama chachu ya hamasa zaidi kikazi na usirudi nyuma.

"Changamoto zipo leo, kesho na keshokutwa hazitokuwepo tena. Jambo unalotakiwa kufanya ni kutazama lengo lako na kufanya bidii kila kukicha kuzikabili changamoto husika, ili ukafikie lengo lako," anasema.

Hilo analitaja, akihamasisha kwamba wajasiliamali wanaotaka mikopo kwa ajili ya kuanzisha biashara au kuendeleza biashara zao.

# Diplomasia Uchumi kwenye sekta Utalii, kukikamilisha yaliyokwishaanza kwa hatua

Inatoka Uk 11

Mnamo Septemba mwaka jana, serikali za Ujerumani na Tanzania zilitiliana saini mkataba wa msaada wenye thamani ya Euro milioni 10 sawa na shilingi bilioni 23.7, kwa ajili ya utekelezaji wa maeneo makuu matatu ambayo ni: Miradi ya kukabiliana na migongano kati ya wanyamapori na binadamu; haki za wanawake na watoto; na maandiko ya kitaalamu ya miradi.

Ni mkataba uliotiwa saini Dar es Salaam, kati ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba kwa niaba ya serikali ya Tanzania na Balozi wa Ujerumani nchini, Regine Hess, kwa niaba ya serikali ya Ujerumani. Hapo Tutuba anafafanua mradi wa kukabiliana na migongano ya wanyamapori na binadamu, umetengewa fedha Euro milioni sita, ambazo zitatumika kupunguza vifo vinavyosababishwa na wanyamapori kwa jamii zinazozunguka baadhi ya hifadhi za wanyamapori na kuepusha uharibifu wa bayoanuai katika hifadhi za wanyamapori.

Huku Rais Dk. Samia akiwa mstari wa mbele kutetea kinamama nchini, nayo inaangukia katika dhana ya maelekezo ya ufafanuzi wa Tutuba, kwamba kuna fedha Euro milioni tatu za Mradi wa Kuwezesha Upatikanaji wa Haki za Wanawake na Watoto.

Anataja mradi wa tatu kwa maelezo; ni wa kuandaa maandiko ya kitaalamu ya miradi, iliyogharimu kiasi cha Euro milioni moja, ambako kunafanyika upembuzi yakinifu wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za misaada kutoka serikali ya Ujerumani.

"Msaada huu ni sehemu ya ahadi ya misaada ya jumla ya Euro milioni 71, sawa na shilingi bilioni 188.65 iliyotolewa na shirikisho hilo, katika majadiliano yaliyofanyika baina ya pande hizi mbili, jijini Dar es Salaam tarehe 25 Novemba 2021 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimaendeleo," anatamka Tutuba.

"Nawahakikishia kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi wa Mheshimwa Samia Suluhu Hassan, itafuata taratibu na kanuni zote za kisheria na kuhakikisha kwamba miradi hii inatekelezwa kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa" anaeleza.

Ni safari iliyoanzia jijini Berlin Ujerumani, ujumbe wa Tanzania ulioongozwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba na ujumbe wa Ujerumani ulioongozwa na Naibu Waziri anayesimamia uhusiano wa kiuchumi na maendeleo wa nchi hiyo, Dk. Barbel Kofler, kuwezesha kupatikana msaada wa shilingi bilioni 210, kwa ajili ya utekelezaji miradi ya sekta za afya, maji, utalii, mazingira, utawala bora, kuwawezesha wanawake kiuchumi na kuboresha mfumo wa kidijitali kwa ajili ya kufuatilia matukio ya ukatili kwa wanawake na watoto.

"Serikali ya Tanzania ina furaha kupokea msaada wa Euro milioni 87, sawa na Sh bilioni 210, utakaosaidia kwa kiwango kikubwa kuboresha maisha ya watu," akatamka Dk. Nchemba, wakati akitoa neno la shukrani baada ya kutiwa saini nyaraka za makubaliano ya msaada huo.

"Msaada huo pia unakusudia kuboresha afya ya mama na mtoto, kuimarisha uzazi wa mpango hususani kwa vijana na mpango wa bima ya afya kwa wote," akaeleza msomi wa uchumi, Dk. Nchemba, akitaja fedha pia zitaelekezwa kusafisha mazingira na uhifadhi salama wa vyanzo vya maji ya kunywa Tanzania Bara na Visiwani.

Nchemba akafafanua zaidi miradi mingine itakayonufaika na fedha hizo kuwa ni mradi wa hifadhi ya mfumo wa ikolojia wa Serengeti, Mradi wa Hifadhi Ikolojia ya Selous na Nyerere, mradi wa Kuboresha Afya Tanzania Awamu ya Pili, akihitimisha na hoja: "Kwa niaba ya serikali ya Tanzania, inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, ninaishukuru Serikali ya Shirikisho la Ujerumani kwa msaada huu mkubwa na nikuhakikishie kuwa tutafuatilia matumizi ya fedha hizi kwa karibu zaidi ili manufaa yaliyokusudiwa yapatikane."

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Siku ya Nyerere itazamwe upya






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

JULIUS Kambarage Nyerere Burito, ni jina kubwa sana Butiama, Mara, Tanzania, Afrika Mashariki, Kusini mwa Afrika, barani Afrika na duniani kwa ujumla.

Mwalimu Nyerere kama alivyokuja kujulikana baadaye, alizaliwa Aprili 13, 1922 kijijini Butiama wilayani Musoma mkoani Mara na akaja kufariki dunia Oktoba 14, 1999 Jijini London, Uingereza.

Baba huyo wa Taifa, amezikwa Mwitongo kijijini Butiama, ambako baadhi ya Watanzania na wasio Watanzania, huenda kuzuru kaburi lake kila wapatapo fursa na kukumbuka mengi aliyowaachia.

Nasi Watanzania wakati anafariki dunia na baada ya kumzika, tuliahidi kumuenzi kwa kutenda na kuendeleza mema aliyotuachia kama jamii, lakini kama wananchi wa nchi aliyoipigania kutoka makucha ya Wakoloni.

Mtanzania yeyote akiulizwa hivi sasa anamuenzi vipi Mwalimu Nyerere, hatakosa la kusema na hasa viongozi ndio kabisa, kwa sababu kuwa karibu tu na Mwalimu hata kinadharia ni karata tosha ya uongozi.

Katikati ya mwezi huu, Watanzania tuliadhimisha miaka 24 ya kumbukizi ya kifo chake, tukiongozwa na Mkuu wa Nchi, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa mjini Babati.

Shamrashamra zilikuwa kubwa, kwani zilikwenda sambamba na tukio la kuhitimisha mbio za Mwenge wa Uhuru, pia hitimisho la Wiki ya Vijana. Mbio hizo zilitawaliwa na kaulimbiu ya kuhifadhi mazingira.

Waliohudhuria maadhimisho hayo na hata waliofuatilia kwenye vyombo vya habari, walishuhudia jinsi shughuli za kuzima Mwenge zilivyoshamiri hata kufunika Siku ya Nyerere.

Mapambo yaliyokuwa uwanjani hapo, sare rasmi zilizovaliwa na wahusika wa maadhimisho hayo wakiwamo viongozi wa kitaifa, yalionyesha picha za kiongozi mkuu wa nchi, Dk Samia pamoja na Mwenge wenyewe, bila picha ya Nyerere kokote.

Hiyo ni pamoja na mabango yaliyozunguka uwanja huo, ambayo nayo yalikuwa na picha hizo hizo, achilia mbali uwakilishi hafifu wa familia ya Mwalimu, ambao ulifanywa na mwanawe wa kiume, Charles Makongoro.

Mimi binafsi nilitarajia, angalau katika waliopewa fursa ya kuhutubia umati uliofurika uwanjani hapo, lakini na Taifa lililokuwa likifuatilia sherehe hizo, basi Makongoro angepewa fursa ya kutoa salamu za familia ya tuliyekuwa tunamkumbuka.

Lakini, salamu nyingi ziliegemea kwenye Mwenge na miradi iliyopitiwa nao mikoani katika siku zote ulizozunguka nchini, jambo ambalo ni jema kwa Taifa na ndiyo sababu hata Makamu wa Rais, Dk Philip Mpango akaomba kaulimbiu hiyo iendelee katika mbio za mwakani na unaofuata.

Watoto wa halaiki halikadhalika nao waliegemea zaidi katika kutoa ujumbe wa Mwenge na maendeleo ya mkoa wa Manyara na nchi kwa jumla, bila kujiegemeza kwa Mwalimu na siku yake.

Hivi karibuni, Rais Dk. Samia aliunda kamati iliyopitia kujua jinsi Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inavyojiendesha na kuomba kujua nini kimejiri na hakika alikipata kwenye taarifa.

Mimi nadhani ipo haja kufanya hivyo kwa wizara zingine, lakini hata taasisi za umma, lakini hata hili la Siku ya Nyerere nalo na kupewa uzito ili iwe siku pekee yenye maudhui yanayomhusu Mwalimu kama Mwalimu na si kuchanganywa na mengine na kufunikwa.

Ni kweli, kwamba Siku ya Nyerere ni ya mapumziko, lakini bado hiyo haitoshi kumheshimisha kutokana na uzito na umuhimu wa mchango wake kwa Watanzania, kwani inahitajika siku maalumu, si tu ya kupumzika, bali kukumbuka kwa vitendo alivyofanya.

Tunayakumbukaje? Ndiyo sababu kuna vikundi kama Twende Butiama, kikundi ambacho kwa miaka mitano sasa kimekuwa kikiendesha baiskeli kutoka Dar es Salaam hadi Butiama, humo njiani kikiamshaamsha watu kumkumbuka Mwalimu.

Tuna vikundi vya ngoma, kwaya, bendi za muziki na vingine, vihamasishwe kutunga nyimbo za kukumbuka mema ya Mwalimu na kuimbwa au kupigwa hata kwa wiki kabla ya siku yenyewe, lakini kuandaa matamasha, warsha, makongamano, semina na mikutano ya kujadili mema yake.

Lakini kama hayo hayawezekani, tujiulize kwanini Siku ya Nyerere iwe ya kufariki dunia na si ya kuzaliwa, kama ambavyo watu wengi huadhimisha siku zao za kuzaliwa na si za kufa? Ndiyo sababu hata mataifa husherehekea siku za kupata uhuru au kujikomboa (Taifa kuzaliwa).

Tukiweza hilo, ina maana Siku ya Nyerere itakuwa Aprili 13 ya kila mwaka na hivyo siku ya kifo itaachwa ibaki ya kuzima Mwenge kwa sababu ndiyo siku ambayo na yeye alizima akiwa kitandani katika hospitali ya Mtakatifu Thomas. Ni ushauri tu ndugu zangu au siyo wajameni!

UCHUMI

# Picha pana ya unyanyasaji kijinsia unavyowatia umasikini mama, mtoto

## •Kukosa ajira nako kunageuza hukumu butu



Sehemu ya mabinti masomoni, kundi linalohitaji ulinzi wa kijamii. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Grace Gurisha**

HADI sasa katika jamii nchini na nje ya mipaka, kuna kilio kwa wanawake na watoto kuonewa. ni tatizo linaloikumba jamii hiyo kwa wingi huku tafiti nyingi zilizofanywa zikionyesha kuwa bado kundi hilo limekuwa likiathiriwa kwa kiasi kikubwa.

Licha ya taasisi mbalimbali ikiwamo Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (Wildaf), zikiendelea kukemea hali hiyo ya ukatili kupungua, lakini bado inaonekana kuendelea kuwepo katika majumba ya watu.

Matukio ya ukatili wa kijinsia nchini Tanzania yanatajwa bado yapo, ikitajwa utatuzi wake ni msingi wa malengo ya maendeleo na nyenzo ya kufikia malengo mengine ya wanawake, familia, jamii na taifa kwa ujumla.

Ukatili pia, unadhorotesha ukuaji uchumi wa wananchi, kutokana na serikali kutumia gharama kubwa kushughulikia athari zake kijinsia, badala ya kujikita katika maendeleo, inabaki kikwazo cha kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030.

Takwimu zilizotolewa na Jeshi la Polisi zinaonesha kuwa kuanzia Januari hadi Juni 2021, watu takribani 1,5131 walifanyiwa ukatili wa kijinsia, huku ripoti hiyo ikionyesha ongezeko la mauaji kwa wanawake walio katika ndoa.

Ripoti iliyotolewa mnamo Septemba 2021 na Jarida la Afrika kuhusu hali ya ukatili wa kijinsia nchini miongoni mwa wanandoa, inaonyesha kuwa asilimia 46 ya wanandoa hufanyiwa ukatili wa kijinsia, kati yao asilimia 36 walifanyiwa wa kimwili na asilimia 32 walifanyiwa wa kisaikolojia, huku asilimia 13 walifanyiwa ukatili wa kingono.

Ukatili wa kijinsia unaelezwa, pale unapofanyika huchangiwa na kuporomoka kwa maadili na changamoto za kiuchumi ndani ya familia, madhara yake yakiangukia kupunguza nguvukazi ya taifa, kuleta umasikini katika familia.

### KUTOKA TGNP

Anna Sangai, Ofisa kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Idara ya Ujengeaji Uwezo na Mafunzo, anasema hali ya ukatili inaendelea kutisha, kwani kwa sasa unaoongoza kuripotiwa ule wa kinamama kutelekezewa familia na waume zao, wakibaki wanahangaika a kutafuta msaada.

Anasema TGNP imekuwa na kituo cha kukusanya taarifa na maarifa vya mkoani Dar es Salaam, ambako hupokea taarifa za ukatili kwa nyakati tofauti.

Sangai anasema, ukatili unaendelea kufanyika, hasa katika maeneo ya pembezoni, ambako watoto wanabakwa na kulawitiwa.

"Tunaziomba serikali za mitaa, kuendelea kuimarisha madawati ya jinsia ambayo kwa asilimia kubwa yamekuwa msaada kwa watu pia ustawi wa jamii, wanapaswa kuimarisha mfumo wao ambao kwa sasa haupo rasmi

'Serikali iimarishe mfumo rasmi wa kuwahifadhi wahanga wa ukatili wa kijinsia. Unakuta mama amepigwa, ameenda kumshitaki (Polisi), akitoka hapo ana kwenda wapi? Kwa hiyo, unakuta anarudi kule kule alipopigwa," anasema. Sangai

Mkurugenzi wa Chama cha Wanawake Wanasheria Tanzania (TAWLA), Tike Mwambipile amesema hali ya ukatili kwa ujumla haijabadilika. Hapo ana ufafanuzi: " Bado watu wanaendelea kufanyiwa vitendo vya ukatili na ukatili, sisi TAWLA kesi tunazozipokea nyingi ni vipigo na kwa sababu ni kosa la jinai."

Aidha, anataja ukatili mwingine kwa sasa unaoripotiwa sana, unaohusu wanawake wanaofanya biashara hali iliyosababisha wawe vizuri kiuchumi, hivyo wenza wao wanaumia na kuona wanadhalaurika.

### MTAALAMU WA SHERIA

Wakili Wigayi Kissandu, anasema ukatili bado upo kwa kiasi kikubwa na unatokana na mazingira ambayo mengine usababisha watoto kutelekezwa na baba zao.

Anasema, kumekuwapo kesi nyingi zinazofunguliwa katika Mahakama ya Watoto, wanaume huwa hawabishi kama sio watoto wao, lakini shida hutokea kwamba wengi sio waajiriwa, kwa hiyo ni ngumu kupata mishahara yao na kuwahudumia watoto.

"Baba akiitwa mahakamani atawaambia kwa mfano atoe Sh 50,000 kulingana na uwezo wake. Sasa kazi ipo kwenye utekelezaji, ni mgumu, lakini mwajiriwa kwake inakuwa rahisi, kwa sababu tunapeleka barua ya kukamata mshahara, kwa hiyo inakuwa rahisi," anatamka Wakili Kissandu

Pia, anasema ukatili wa majumbani nao ni changamoto kubwa, kwani wanaotaka kuvunja ndoa, unakuta baba katelekeza ndoa yake na kuhamia 'nyumba ndogo'.

Kuhusu kesi za mirathi,Wakili Kissandu anasema, hizo za mirathi nazo zimekuwa nyingi, huku kukiwapo ongezeko la wajane, kwa sababu mume anapokufa, ndugu zako wanaona mali ni za kwao, wakiwakosesha mjane na watoto haki zao za msingi.

"Takwimu tulizo nazo mwaka jana tulikuwa na maombi ya talaka 532, kutunzwa watoto wa ndoa/ wanandoa 113, kutengana 67, kesi za mirathi 427 na matunzo ya watoto 418,"anasema .

### ALIYEATHIRIWA

Mmoja wa waathirika katika ukatili wa kijinsia (jina tunalo), Amina Athuman, anasimulia asilolisahau katika maisha yake, kitendo alichofanyiwa na wazazi wake kumkeketa, hata kumsababishia hana furaha na ndoa yake.

"Mimi ni mama wa miaka 43 nina watoto watatu, katika miaka yote hiyo sikuwahi kufurahia tendo la ndoa kutokana tu na kiungo changu kilichopunguzwa kwa mwili wangu na sikuwahi kufikishwa yaani inauma sana," anasema.

Hapo Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia wanawake na Makundi Maalum, Dk Dorothy Gwajima, anajumuisha hoja kwamba bado serikali inaendelea kupambana na changamoto za ukatili wa kijinsia, kuhakikisha usawa unapatikana na kila mtoto na mwanamke anakuwa na haki ya kuishi.

Pia, anasema serikali inaendelea kuchukua hatua za kuondoa ukatili, akitaja masuala kama ya ukeketaji, kuna mkutano unaoendelea nchini wa kimataifa, ukiwa na ajenda inayounganishwa na na changamoto za mtoto wa kike.

"Bado tunapambana na fikra za jamii kumuona mtoto wa kike kama chanjo cha utajiri na sio binadamu mwenye haki zake. Mambo mengine ni uelewa tu.

"Unakuta mzazi hakupata fursa ya kwenda shule, haelewi dunia inavyobadilika ili abadilike na kuipeleka familia yake sawa na maendeleo ya kisasa anadhani kushikilia ule msimamo wa nyuma ni sawa,"anaeleza

Dk. Gwajima anasema, serikali inapambana na mila na desturi mbalimbali na bado kuna Watanzania wameshikilia mila na desturi wanazorithi, ambazo hazina faida kwa afya yao na mtoto.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima. **PICHA: GRACE GURISHA**



## Watumishi wafunzwa mfumo mpya ununuzi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) inaendelea kutoa mafunzo kwa taasisi za umma kuhusu matumizi ya mfumo wa ununuzi wa kielektroniki (NeST) na hadi sasa taasisi 802 zimeshafikiwa.

Akizungumza ofisini kwake jana, Mkurugenzi wa Huduma za Ushauri na Kujenga Uwezo wa PPRA, Mhandisi Amin Mcharo, alisema mafunzo kwa watumishi wa taasisi za umma kuhusu matumizi ya mfumo wa NeST yanaendelea na kwamba washiriki 8,435 kutoka taasisi hizo wameshapatiwa mafunzi.

"Mpaka Oktoba 28, 2023 tumekuwa na orodha ya jumla ya washiriki 8,435 waliopatiwa mafunzo ya matumizi ya mfumo, washiriki hao ni wa kutoka katika taasisi za umma 802," alisema.

Mcharo alisema idadi hiyo ni sawa na wastani wa robo tatu ya taasisi zote zilizojisajili kwenye mfumo kati ya 1,042 zilisosajiliwa.

Aliwataka wakuu wa taasisi za umma ambao hawajapata mafunzo kupeleka watumishi wao PPRA kupata mafunzo yatakayowajengea uwezo wa kutumia mfumo wa NeST kwa ufanisi zaidi.

"Kupatiwa mafunzo na wawezeshaji kutoka nje ya PPRA kunaweza kupunguza ufanisi wa mafunzo hayo kutokana na baadhi ya wawezeshaji wa nje kupotosha kwa kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu matumizi ya mfumo wa NeST.

"Niwaombe wakuu wa taasisi za umma kuwatumia wawezeshaji kutoka PPRA ili kuendesha mafunzo kuhusu matumizi ya mfumo, kwani kutumia wawezeshaji wanaotoka nje ya PPRA kwa kiasi kikubwa kunahatarisha ufanisi wa mafunzo, kwa sababu baadhi ya wawezeshaji wa nje hawana uelewa wa kutosha juu ya matumizi sahihi ya mfumo wa NeST," alisema

Alisema miongoni mwa kasoro zonazojitokeza katika uendeshaji mafunzo hayo ni baadhi ya watumishi waliopendekezwa kushiriki kutofika mafunzoni au kufika nje ya wakati.

Hata hivyo, alisema PPRA inaendelea kutoa mafunzo ya mfumo wa NeST katika vituo mbalimbali vilivyo chaguliwa ili kuhakikisha wadau wote muhimu wanautumia mfumo ipasavyo.

# Bil. 1.6/- kukamilisha miradi ya elimu, afya

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

SERIKALI imeipatia Sh. bilioni 1.6 Halmashauri ya Wilaya ya Itigi mkoani Singida kukamilisha miradi ya afya na elimu.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Hussein Simba, alisema hayo juzi kwenye kikao cha robo ya kwanza cha Baraza la Madiwani cha kujadili mambo mbalimbali ambacho kilikuwa na ajenda nane.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. milioni 700 zitatumika kununulia vifaa tiba kwa ajili ya hospitali ya wilaya, vituo vya afya na zahanati.

Simba alisema Sh. milioni 100 zitajenga zahanati mbili, hivyo kuongeza idadi ya zahanati hizo kufikia nane na kwamba Sh. milioni 500 zitatumika kujenga jengo la kufulia, jengo la mionzi na dawa katika hospitali ya wilaya.

Pia alisema sh. milioni 180 zitatumika kwa ajili ya kuziboresha shule 10 kongwe na Sh.Milioni 128 zinakwenda kujenga bweni kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu.

Alisema Sh. milioni 544 zitajenga Shule ya Sekondari ya Majengo na zitakazosalia zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa matundu 20 ya vyoo katika shule mbalimbali zilizoko katika halmashauri hiyo.


Aidha, Simba alisisitiza kwamba halmashauri hiyo imekuwa ikikusanya maradufu zaidi ya mapato ikilinganishwa na awali ambapo mpaka sasa kiasi kilicho kusanywa kinafikia asilimia 54 na kuwa matarajio yao hadi itakapofikia robo ya tatu watafikisha asilimia 100.

Simba alipongeza juhudi za serikali hali ambayo imeonyesha ushirikiano uliotukuka kwa halmashauri hiyo katika muktadha chanya wa ustawi wa maendeleo ya watu.

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Leila Sawe, na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Wilaya hiyo, Jumanne Ismail, walisisitiza halmashauri hiyo kusimamia ipasavyo matumizi ya fedha zote zinazotolewa na Serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, John Mgalula, akizungumza kwenye kikao hicho alipokea ombi la Diwani wa Kata ya Rungwa, Said Yahaya ambaye aliomba asilimia 40 ya mapato yanayokusanywa katika halmashauri hiyo yawe yanapelekwa kwenye kata kwa ajili ya kutekeleza miradi inayoibuliwa na wananchi.

Yahaya alitolea mfano wa stendi ya mabasi ya kata hiyo ambapo Mgalula alisema jambo hilo litapitiwa kwenye kamati ya fedha kuona namna ya kufanya na kueleza kuwa kabla ya kamati hiyo kukaa atawatuma madiwani wa viti maalumu kwenda kuangalia mradi huo.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Itikadi na Uenezi, Paul Makonda, ofisini kwake Bungeni jijini Dodoma, jana**. PICHA: OWM.**

# Kampeni kutangaza kazi serikali yazinduliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMPENI ya Tumewasikia Tumewafikia ambayo inawataka wakuu wa mikoa yote na wakurugenzi wa halmashauri zote 184 nchini, kuandaa mikutano na vyombo vya habari ili kutangaza kwa wananchi kazi zinazofanywa na serikali imezinduliwa rasmi.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Nape Nnauye, akizindua mikutano ya wakuu wa mikoa, wakurugenzi na vyombo vya habari jijini hapa jana alisema pamoja na kazi kubwa inayofanywa na serikali ya awamu ya sita wananchi bado hawana taarifa za kutosha.

Nnauye alisema anaipongeza Idara ya Habari (Maelezo) kwa ubunifu huo na kuja kampeni hiyo ambayo wakuu wa mikoa na wakurugenzi wa halmashauri nchini wataitumia kuandaa mikutano na vyombo vya habari.

"Programu hii ya Tumekusikia Tumekifikia, itakwenda nchi nzima. Lengo lake ni kufahamisha umma kazi kubwa iliyofanywa na inayoendelea kufanywa na serikali kwenye sekta za maji, afya, miundombinu na miradi mingine ya maendeleo nchini," alisema.

Pia alisema lengo lingine la kampeni hiyo ni kuongeza chachu ya mawasiliano kati ya wananchi na serikali yao kwa kuwa itatoa nafasi ya wakuu wa mikoa pamoja na wakurungezi kueleza mambo ambayo yamefanywa.

"Serikali inatoa fedha nyingi za utekelezaji wa miradi mbalimbali hivyo wananchi wanayo haja ya kufahamu kodi zao zinafanya nini tunapozungumzia, maji na afya, lazima wananchi wafahamu nini kinaendelea.

"Tumekuwa na utaratibu wa kufanya mikutano hii katika ngazi za wizara na taasisi hivyo mikutano hii itasaidia wananchi wa ngazi ya chini kabisa kufahamu nini serikali yao inafanya na huko ndiko pia serikali imekuwa ikipeleka kiasi kikubwa cha fedha katika utekelezaji wa miradi mbalimbali," alisema.

Nnauye pia alisema kupitia kampeni hiyo, wananchi watapata fursa ya kueleza kile ambacho serikali yao imefanya na kimewanufaisha kwa namna gani.

Alitoa wito kwa wakuu wa mikoa, wakurugenzi wa halmashauri kutoa ushirikiano kwa Idara ya Habari (Maelezo) ili kupata maudhui mazuri yatakayotumika katika vyombo vya habari.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo) Mobhare Matinyi, alisema lengo la kuanzishwa kwa kampeni hiyo ni kuwafikisha wananchi ngazi ya chini taarifa kuhusu kazi inayofanywa na serikali yao.

"Hivi sasa serikali inafanya mambo makubwa sana katika maeneo mbalimbali lakini ukiangalia ukubwa wa kazi unaofanywa na taarifa zinavyosemwa ni mbigu na ardhi.

"Hivyo kampeni hii itasaidia kufikisha taarifa sahihi kwa wananchi kuhusu kile kinachofanywa na serikali yao na kuondoa 'gap' lililopo hivi sasa baina ya serikali na wananchi wake" alisema.

Matinyi alisema kampeni hiyo baada ya kuzinduliwa jijini hapa jana itakwenda katika mikoa yote na halmashauri zake zote 184 nchini ambapo awamu ya kwanza itakuwa ni mikoa ya Dodoma, Morogoro, Pwani na Dar es Saalam.





# Madiwani wadaiwa kuingilia majukumu watendaji

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

BAADHI ya madiwani wa Halmashauri ya Busokelo, Rungwe mkoani Mbeya wanadaiwa kuingilia majukumu ya utendaji ya watumishi wa halmashauri hiyo hali ambayo inawakatisha tamaa na baadhi yao kuanza kuomba kuhama.

Madiwani hao wamedaiwa kuwa wamekuwa wakivuka mipaka ya kazi zao kwa kutoa maagizo kwa watumishi wa kada mbalimbali yanayowataka kutimiza matakwa yao badala ya miongozo ya kazi zao na wanapokataa, wanaazimiwa kuchukuliwa hatua.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Jaffar Haniu, aliwaonya madiwani hao alipotoa salamu za serikali kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani na kusema baadhi ya madiwani hao wamekuwa wakikataa kufanya kazi na watumishi hao kwa madai ya kutosikilizwa.

Alisema serikali inaajiri watumishi wa kada mbalimbali kwa kuzingatia uwezo wao ili kuondoa upungufu wa watumishi pamoja na kurahisisha utendaji kazi kwenye halmashauri hiyo, hivyo akasisitiza kwamba kuwakataa ni kukwamisha huduma kwa wananchi wao.

"Jambo hili si jema na ni kinyume cha taratibu za utumishi wa umma. Madiwani mnayo mipaka yenu katika ufanyaji kazi lakini cha kusikitisha baadhi yenu mmekuwa mkiwakataa watendaji hawa, mnachagua watu wa kufanya nao kazi kwa maslahi yenu. Acheni mara moja tabia hiyo," alisema Haniu.

Alisema kuna baadhi ya majukumu ambayo hayahitaji siasa kwenye utekelezaji wake bali yanahitaji utaalamu, hivyo ni vyema madiwani wakawaachia wataalamu.

Pia aliwataka madiwani katika halmashauri hiyo kusimamia miradi ya maendeleo kwa kuhakikisha inatekelezwa kwa wakati na kwa ubora kulingana na thamani ya fedha ili kuisaidia serikali kutimiza dhamira yake ya kuwahudumia wananchi. Katika hatua nyingine, Haniu aliwataka wakusanyaji wa mapato katika halmashauri hiyo kuwa waaminifu kwa kuwa wako baadhi wanaingilia mifumo ya ukusanyaji mapato kwa lengo la kufanya ubadhirifu na kwamba wameshaanza kuwachukulia hatua.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Busokelo, Loema Peter, alisema serikali inaendelea na ukamilishaji wa miradi ya maendeleo katika halmashauri ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya, miradi ya elimu na miundombinu ya Barabara hivyo akataka ushirikiano kwa madiwani katika usimamizi.

Alisema miradi hiyo inatekelezwa kwenye maeneo ya kata na vijiji ambako ndiko walipo wananchi na hivyo akawataka madiwani ambao ndio wenyeviti wa kamati za maendeleo kusaidia kwenye usimamizi.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Lusajo Kalla, aliwataka madiwani kwa kushirikiana na maofisa maendeleo ya jamii na watendaji kufuatilia vikundi vilivyokopeshwa mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri ili fedha hizo zirudi na kukopeshwa kwa wengine.



Daktari Bingwa wa magonjwa ya Saratani kutoka Taasisi ya Saratani ya Ocean Road Dk. Sadiq Siu (kushoto), akitoa mada juu ya saratani ya matiti, saratani ya mlango wa shingo ya kizazi na ya tezi dume kwa wafanyakazi wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya benki hiyo kuadhimisha mwezi wa saratani ya matiti kwa kutoa elimu kwa wafanyakazi wake na kuwafanyia vipimo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumia moto kisa kusafisha mashamba

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MAOFISA watendaji kata na vijiji katika wilaya ya Ludewa mkoani Njombe, wametakiwa kuweka ulinzi mkali ili kuwabaini watu wanaowasha moto ovyo kwa lengo la kusafisha mashamba.

Akizungumza katika kikao cha baraza la madiwani, Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya hiyo, Wise Mgina, alisema uchomaji moto usiofuata taratibu unasababisha madhara katika baadhi ya maeneo ikiwamo kuunguza nguzo za umeme.

"Nitoe rai kwa wananchi wa wilaya ya Ludewa tuache hii tabia ya kuchepusha moto na niwaombeni sana watendaji wa kata tupo hapa, tukirudi kule tukashirikiane na watendaji wa vijiji na wenyeviti tulisimamie vizuri hili suala la moto kwa sababu linaleta hasara kubwa,' 'alisema.

Mgina alisema kutokana na changamoto hiyo kuna baadhi ya maeneo hadi hivi sasa hayana umeme.

"Mpaka tunazungumza hapa kuanzia Lupingu hakuna umeme inakaribia siku ya tano au ya sita kwa sababu ya utoroshaji wa moto na kuna mito mingi imeungua maeneo hayo," alisema Mgina.

Alisema ni vizuri wananchi wakaelimishwa kwamba wanavyotorosha moto wanasababisha madhara makubwa pamoja na hasara.

Diwani wa Ludende, Vasco Mgimba, alisema katika kata yake tayari ameshaweka mikakati ya kupamba na janga la moto.

"Mkakati wa kwanza ni kudhibiti moshi, yaani tunapoona moshi unavuka mahali fulani basi wananchi wachukue jukumu pamoja na kamati za vitongoji kwenda kuchukua hatua kwa sababu moshi ni kisababishi cha moto. Unapochoma moto mchana kuna athari kubwa, tunakosa umeme, kuna nguzo zinateketea kabisa," alisema Mgimba.

Diwani wa Lupingu, Jackson Mwankenja, alisema chanzo kikubwa cha kuchoma moto ni wananchi kuandaa mashamba na matukio hayo yanakuwa mengi hasa kipindi hiki kuelekea msimu wa kilimo.

# Bil. 21/- kujenga barabara mitaa jiji Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Miji Tanzania (TACTIC) imetoa zaidi ya Sh. bilioni 21 kwa ajili ya ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 12 kwa kiwango cha lami katika mitaa mbalimbali ya jiji la Mbeya.

Akizungumza wakati wa mkutano wa kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo uliofanyika jana jijini hapa, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, aliwataka madiwani ambao mradi utapita katika maeneo yao, kushirikiana na serikali kwenye usimamizi.

Pia aliwataka madiwani hao kuwashirikisha wananchi katika kila hatua ya utekelezaji ili na wao wafahamu kinachoendelea na hata kushiriki kwenye utekelezaji.

Aliwaomba wananchi wa jiji hilo kutoa ushirikiano kwa makandarasi wa mradi huo pamoja na kushirikiana na wasimamizi wa mradi kudhibiti wizi wa vifaa vya mradi huku akiwataka makandarasi kuwapa kipaumbele cha ajira wananchi wa maeneo husika.

"Wananchi walikuwa na shauku ya kuona mradi huu unaanza kutekelezwa. Sasa nendeni mkawaambie tunaanza kazi na kuwaeleza namna watakavyonufaika ili watupe ushirikiano husasani kwenye ulinzi wa vifaa vya mradi," alisema Malisa.

Alimtaka mkandarasi aliyepewa zabuni hiyo kujenga barabara hizo katika ubora wa hali ya juu na kukamilisha ndani ya miezi 15 kama walivyokubaliana kwenye mkataba ili wananchi waanze kunufaika.

Mwakilishi wa Kampuni ya Mhandisi Consultant ambayo ndiyo imepata tenda ya kuwa mkandarasi mshauri kwenye mradi huo, Jofrey Kanjanja, alisema awamu ya kwanza ya ujenzi inatarajiwa kuanza mapema mwezi huu na kwamba itahusisha ujenzi wa barabara tano pamoja na mitaro miwili.

Kanjanja alisema barabara zitakazojengwa na urefu wake kwa kilomita kwenye mabano ni Uyole - Itezi (1.8), Iziwa (mbili) Kabwe - Block T- SIDO (1.2), Ilomba-Machinjioni (3.8), Kalobe (3.5) na mitaro miwili katika eneo la Nzovwe na Iyela yenye urefu wa kilomita sita.

Aliishukuru serikali kwa kuwaamini makandarasi wazawa kuwapa ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kuahidi kutekeleza ujenzi wa barabara hizo kwa kiwango cha ubora sawa na thamani ya gharama husika za mradi huo.



## Wanafunzi wapya SUZA wafundwa

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Prof. Mohamed Makame Haji, awewataka wanafunzi wapya wanaojiunga na chuo hicho kutimiza malengo yao ya kusoma kwa bidii ili kuwa wataalamu kupitia nyanja mbalimbali.

Akizungumza na wanafunzi wapya wa chuo hicho katika wiki ya maandalizi ya mwaka wa masomo 2023/24 katika ukumbi wa Dk. Ali Mohammed Shein, Tunguu, Prof. Mohamed alisema mipango ya chuo hicho ni kutoa msukumo katika fani mbalimbali na kuimarisha miundombinu ili kiendelee kuaminika na kujenga soko la ajira.

Lengo la chuo hicho, alisema ni kuimarisha vijana kupata ujuzi, taaluma na stadi mbalimbali zinazotolewa ili kuwa wabunifu ambao watakuwa na sifa ya kuajika na kujiajiri.

Prof. Mohamed alisema chuo hicho kina mpango wa kuimarisha elimu nchini na kutengeneza uwezo wa uhitimu ambao utakuwa na vigezo vya kuwa na utaalamu wa kutumia sayansi na teknolojia katika maeneo yanayowazunguka ili vijana wanapotoka waweze kuchangia maendeleo ya nchi.

Pia alisema mipango hiyo imelenga kuhakikisha kinaendana na malengo ya serikali katika kuwaandaa watalaamu watakaosaidia katika masuala ya kuimarisha uchumi.

Aliwataka wanafunzi kutumia mazingira salama kwa usahihi wake na kupokea taaluma wanazozihitaji katika fani mbalimbali ili kupata watalaamu na kufanya utafiti utakazosaidia kuleta mabadiliko ya chuo na taifa kwa ujumla.

Makamu mkuu huyo aliwapongeza wanafunzi hao waliopata nafasi ya kujiunga na chuo hicho na uwepo wao utawapa nafasi na watendaji wa chuo hicho ambayo ndio yatakuwa sehemu ya maisha yao katika miaka yote ya uwapo wao chuoni.

Alisema safari hiyo kila mmoja angetamani kuipata lakini fursa wameipata wao ambao ni sehemu ya vijana walioomba kujiunga na chuo walikuwa 8,575 kutoka maeneo mbalimbali na waliobahatika ni 4,484 kutokana na sifa walizo nazo.

Ofisa Masoko na Uhusiano Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Salim Hassan Iddi, alisema benki hiyo imekuja na mikakati maalum ya kuwawezesha wanafunzi wa elimu ya juu kupata huduma kwa urahisi wakati wote.

Alisema wameamua kuja na akaunti maalum ambayo wanafunzi kuanzia sasa kupitia benki hiyo wataweka fedha zao bila ya kuwa na makato na kupatiwa kadi za ATM bure ikiwamo ya kawaida na Visa Card.

Hassan Khairallah Tawakal, msaidizi wa mkuu wa ustawi wa wanafunzi wa chuo hicho alipongeza PBZ kwa hatua za kuwapa wepesi wanafunzi katika kupata huduma ili wasome vizuri na kuepukana na changamoto na vishawishi ambavyo vinawakatisha safari yao ya masomo.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake, Ali Khatib Abass alisema huduma za PBZ vyuoni kwa kiasi kikubwa zitarahisisha huduma kwa wanafunzi na kusoma bila usumbufu na mara nyingi mikopo imekuwa ikichelewa.

# Wamiliki wa machinjio wahimizwa usafi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAMILIKI wa machinjio ya nyama wametakiwa kuhakikisha yanakuwa safi, ili kuepusha maradhi kwa jamii.

Hayo yalisemwa visiwani hapa na Mkurugenzi wa Udhibiti na Usalama wa Chakula kutoka Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi, Dk. Khamis Ali Omar, wakati akifungua mafunzo ya siku moja yaliyowashirikisha wamiliki wa machinjio, wachinjaji na wasafirishaji wa nyama.

Alisema hali ya usafi katika machinjio yote hairidhishi, hivyo ni rahisi kupata maradhi ambayo yatanzia kwenye machinjio na kuishia kwa walaji kutokana na eneo la utayarishaji kutokuwa salama.

Kuna maradhi mbalimbali yanaweza kutokea yakiwamo kutoka kwa wanyama Kwenda kwa binadamu lakini kama kutakuwa na utaratibu mzuri maradhi hayo yatadhibitiwa.

"Tumeamua kuja hapa kupeana mafunzo kwa wadau wa machinjio na wasafirishaji wa nyama kwa lengo la kulinda afya ya jamii," alisema.

Dk. Khamis aliwataka wadau kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa, kusafirishwa zinakuwa salama kwa watumiaji na kuhakikisha machinjio hayo yanakuwa safi na kufuata vigezo vilivyotolewa kisheria juu ya kuanzisha machinjio hayo. Kinyume cha hayo, alisema watachukuliwa hatua.

Alisema matarajio ya baadaye, magari ambayo yanasafirisha nyama yawe na viyoyozi ili kuwe na ubaridi na hilo ni takwa la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Wakitoa mada kuhusu mwongozo wa machinjio Daktari wa Mifugo, Thamra Khamis na Mwajuma Kombo Ali, ambaye ni Mkaguzi wa Chakula katika Wakala wa Chakula na Dawa Zanzibar (ZFDA), walisema lengo la mafunzo hayo ni kwenda kufanya marekebisho majengo ya machinjio yao na magari ambayo yanasafirisha nyama ili kujiandaa na usajili ambao utaanza mwezi huu.

Ofisa kutoka Wizara ya Kilimo na Mifugo, Dk. Othman Juma, akiwasilisha mada kuhusu Kanuni ya Nyama ya Mwaka 2015, alisema kanuni hiyo ni maalumu kwa ajili ya kusimamia nyama, ambayo imekusanya vitu vingi vya msingi.

Alisema kanuni hiyo imewekwa ili taratibu zifuatwe kwa lengo la kulinda afya ya jamii na haki za wanyama na kuwataka wadau hao waongeze uwelewa juu ya umuhimu wa ukaguzi wa nyama ili wafikie pahala pazuri na kubadilisha sekta hiyo na kuifanya iwe bora na salama kwa afya zao.

Wakichangia katika mafunzo hayo, Haroub Abdalla Suleiman, kutoka machinjio ya Kisakasaka, alisema pamoja na kuwa wamepatiwa mafunzo kuhusu haki za wanyama ni wajibu wa hata wale wanaofuga mitaani ambao wamekuwa wakionekana kuwatesa.

Kuhusu wanyama wanaotoka Tanzania Bara ambao kisheria wanatakiwa kuchukuwa muda kabla ya kuchinjwa, alisema hawana maeneo ya kutosha ya kuwahifadhi, hivyo kusababisha kuibwa.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akichagua viatu baada ya kufungua soko la wajasiriamali la Chakechake, Pemba jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makumbusho Zanzibar, Bara kushirikiana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

IDARA ya Makumbusho na Mambo ya Kale Zanzibar na Makumbusho ya Taifa ya Tanzania, zimetiliana saini hati ya ushirikiano kuhusu usimamizi na uendeshaji wa makumbusho na maeneo ya kihistoria ya pande hizo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Naibu Katibu Mkuu Wizara Utalii na Mambo ya Kale, Dk. Amina Ameir Issa, alisema hatua hiyo itasaidia kushirikiana katika shughuli mbalimbali kwa lengo la kuyaendeleza maeneo hayo.

Pia alisema hatua hiyo itasaidia watendaji na wafanyakazi wa taasisi hizo kupanua wigo kwa kushirikiana katika nyanja mbalimbali za kiutendaji na kuyatangaza maeneo hayo ndani na nje ya nchi.

Naibu Katibu Mkuu huyo alisema makubaliano hayo pamoja na mambo mengine, yatatoa matokeo chanya kwa kuyaendeleza maeneo hayo kufanya utafiti sambamba na kuyahifadhi ili kukuza uchumi wa nchi kupitia utalii wa urithi.

Mkurugenzi Mkuu Makumbusho ya Taifa, Dk. Noel Lwoga alishukuru kukamilika mkataba huo kwa sababu mashirikiano ya taasisi hizo yalianza zamani na shughuli mbalimbali zilikuwa zikifanyika lakini yalikuwa si rasmi, hivyo kupitia hatua hiyo yameleta sura nyingine.

Alisema, hatua hiyo ni chachu ya kufanikisha uendeshaji wa maeneo hayo kwa kupatikana rasilimali mbalimbali ikiwemo fedha na mambo mengine kwa ajili ya kuyaendesha ili kuchochea uchumi wa taifa.

Mkurugenzi wa Makumbusho na Mambo ya Kale Zanzibar, Maryam Mohammed Mansab, alisema idara hiyo imeweka mikakati ili kuhakikisha sekta hiyo inaimarika na kuwa chachu ya kuleta tija hapa nchini.

Alisema hatua hiyo ni moja ya kudumisha na kuendeleza Muungano kwa lengo la kuona kila mmoja ananufaika na rasilimali hizo kwa maslahi mapana ya kizazi cha sasa na cha badaye.

Akizungumzia baadhi ya maeneo ambayo watashirikiana, alisema ni pamoja na uhifadhi wa kisayansi kwa mikusanyo ya makumbusho, uhifadhi wa majengo ya kale, usajili wa kidigitali kwa mikusanyo ya makumbusho na mambo ya kale, uandaaji wa matamasha na maonyesho na maeneo mengine mbalimbali.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**HOSEA BETHUEL KINTINGU** anatangaza kupotea kwa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0361-0154 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SINGE SECONDARY SCHOOL MWAKA 2017** na cheti cha chuo cha **ORDINARY DIPLOMA IN CLINICAL MEDICINE NTA LEVEL 6** chenye usajili namba **NS0361/0154/2017** kilichotolewa na **TANDABUI INSTITUTE OF HEALTH SCIENCES AND TECHNOLOGY** mwaka 2021. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DOD/DOD/RB/204524/2022**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 137 OF 2023**

**In the matter of the Estate of the late COSMAS ARON SALINGWA of Kikuyu within Dodoma City**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY BAHATI JUMA SAHAYA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 22 Day of November,2023

Dated at Dodoma this 02 Day of November, 2023.

COURT SEAL DODOMA

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**(SHAURI LA MAOMBI YA MADAI HALISI Na. 104 YA 2023)**

**SCANCEM INTERNATIONAL D.A............................MDAI NO.1**
**FAYAZ BHOJANI...................................................MDAI NO. 2**
**HAKAN GURDAL..................................................MDAI NO.3**

**DHIDI YA**

**RASHID SAADALLAH...........................................MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

**RASHID SAADALLAH,**
**S.L.P**
**DAR ES SALAAM**

Kwa kuwa mdai aliyetajwa hapo juu, amefungua shauri la madai dhidi yako, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati za madai zinazopatikana katika mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria, siku ya tarehe 16/11/2023 saa tano (5:00) kamili asubuhi mbele ya MHE.J.D **LUAMBANO – DR** kujibu madai dhidi yako. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia katika utetezi wako siku hiyo.

**ANGALIZO:** Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na mahakama ikithibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.

HATI hii imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya Mahakama leo hii tarehe 16 /10/2023 16/10/20

THE HIGH COURT OF TANZANIA

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
KANDA YA DAR ES SALAAM.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI /TARAKA/MIRATHI NAMBA 220/2023**

**MDAI:RAHMA ABDALLAH HASANI**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: REHEMA MAKALA KINDEMILE**

**KWA; REHEMA MAKALA KINDEMILE**
**WA MOROGORO MANSPAA**

**OMBI LA MDAI : RAHMA ABDALLAH HASANI**
**MADAI YA PESA TSH.6,000,000/=**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri lilimepangawa kusikilizwa mnamo tarehe **07 Mwezi 11 Mwaka 2023** saa **2:30 Asubuhi .**

**Angalia** kama hukudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii inaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 01/11/2023

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 10 YA MWAKA 2023**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**
**RICHARD MANASE KIJO.........................MAREHEMU**
**AMINI RICHARD KIJO..............................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 14 mwezi NOVEMBA, Mwaka 2023.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 1 Mwezi NOVEMBA Mwaka 2023

DISTRICT COURT MWANGA

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA
Hakimu Mkuu Mkazi Mfawidhi
Mwanga

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**EVINES DAMIAN DOMISIAN** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0667/0023/2020** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **NYAISHOZI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI **PHQ/KAG/KAR/3072/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 15 YA MWAKA 2023**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**
**LILIAN NDOLE MSOFE.........................MAREHEMU**

**SERAPIA MARKO EVAREST NA ELIZABETH MARKO EVAREST................................................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 14 mwezi NOVEMBA, Mwaka 2023.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe **1 Mwezi NOVEMBA Mwaka 2023**

DISTRICT COURT MWANGA

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA
Hakimu Mkuu Mkazi Mfawidhi
Mwanga

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 13 YA MWAKA 2023**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**
**SR. MARTINA PETER MSUYA............... MAREHEMU**

**SR.PRISILA MICHAEL SHAYO.................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 14 mwezi NOVEMBA, Mwaka 2023.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe **1 Mwezi NOVEMBA Mwaka 2023**

DISTRICT COURT MWANGA

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA
Hakimu Mkuu Mkazi Mfawidhi
Mwanga

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA 200/2023**

**MDAI:BAHATI MAKUNGU**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: HAMISI NUNDA**

**KWA; HAMISI NUNDA**

**OMBI LA MDAI : BAHATI MAKUNGU**
**MADAI YA PESA TSH.233,000=**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri lilimepangawa kusikilizwa mnamo tarehe 06 Mwezi 11 Mwaka 2023 saa 2:30 Asubuhi .

Angalia kama hukudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii inaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 30/10/2023

..........................................
**HAKIMU**
**MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**MOROGORO**

---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

**0745 700 710.**

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mfumo wa kidijitali taarifa za usalama barabarani wazinduliwa

Na Mwandishi Wetu

JESHI la Polisi na Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), wamezindua mpango wa usalama barabarani kwa kutumia simu kukusanya, kuchakata na kutoa taarifa na takwimu za askari wa usalama barabarani nchini.

Programu hiyo mpya ya simu ya mkononi itaruhusu askari wa usalama barabarani kuandika na kupakia taarifa za matukio moja kwa moja kwenye seva, lengo likiwa kwenda kidijitali.

Mkurugenzi wa Usambazaji wa TBL, Nancy Riwa, alikizungumzia mfumo huo, alisema juzi: "Hii itawezesha jeshi kuondokana na mifumo ya sasa, ambapo taarifa hukusanywa katika vituo vya polisi kimojakimoja, na hatimaye kukusanywa kwa wilaya, mkoa na baadaye kitaifa.

"Kwa ufikiaji wa data ya wakati halisi, mipango na usimamizi wa usalama barabarani utakuwa sahihi na mzuri zaidi. Zaidi ya hayo, madereva pia watafaidika kutokana na kuharakisha kwa madai ya bima, kupunguza muda na utata unaohusishwa na taratibu hizo." Nancy alisema kampuni hiyo inaona fahari na heshima kuwa sehemu ya mpango huo muhimu ambao utakwenda kurahisisha utendaji kazi.

"Tunatambua mchango wao wa busara katika uundaji wa programu. Huu ni mwendelezo wa historia ndefu ya ushiriki wetu katika usalama barabarani nchini, na tunapenda kusisitiza tena dhamira yetu ya kuendelea kusaidia Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani na wadau wengine kuhakikisha tunajenga mifumo imara na madhubuti ya usalama barabarani katika nchi hii, ili kupunguza ajali na matumaini siku moja kukomesha vifo vitokanavyo na ajali barabarani zinavyoweza kuzuilika."

Mwanasheria na Mratibu wa Mafunzo wa Kikosi cha Usalama Barabarani Tanzania, SSP Deus Sokoni alishukuru kwa msaada ambao Jeshi la Polisi Tanzania linapata na jukumu lililopo katika kuwawezesha kutekeleza majukumu yao.

Akifungua mafunzo hayo, SSP Sokoni alisema: "Ukusanyaji wa takwimu sahihi na kwa wakati una umuhimu mkubwa wakati wa kupanga, kufuatilia na kutathmini afua za usalama barabarani na pia kwa ajili ya utendaji kazi wa wadau mbalimbali."

Mkuu wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, SSP Solomon Mwangamilo alisema: "Ninapenda kuwashukuru TBL kwa kupaza sauti zao na kushirikiana na Jeshi la Polisi, hii itaimarisha sana usimamizi wa sheria kwa watumiaji wote wa barabara na kuleta utendaji hadi kiwango cha dijitali.


SALAMU ZA PONGEZI

KISHINDO CHA MIAKA 3 OFISINI

Kamishna Mkuu, Uongozi na Wafanyakazi wa mamlaka ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya zanzibar wanaungana na Watanzania wote kumpongeza Mheshimiwa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutimiza miaka mitatu ofisini kwa mafanikio Makubwa .

*ZANZIBAR BILA DAWA ZA KULEVYA INAWEZEKANA*



Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA KUSIMAMIA UVUVI WA BAHARI KUU

(DSFA)

DSFA DEEP SEA FISHING AUTHORITY TANZANIA

HONGERA KWA MIAKA 3 YA KISHINDO

2020 - 2023

Menejimenti na Wafanyakazi wote wa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu inaungana na wananchi wa zanzibar kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi pamoja na wananchi wote katika kuadhimisha miaka 3 ya uongozi wake uliotukuka.

"uchumi wa bluu kwa uvuvi endelevu. "



Mh Dk Hussein Ali Mwinyi
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

MAWASILIANO
Tovuti: www.dsfa.go.tz
Email: info@dsfa.go.tz, S.L.P 56 Zanzibar - Tanzania

# COASTAL, NAMUNGO MAMBO MAGUMU

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kupata ushindi katika michezo yao iliyopita, klabu za Coastal Union na Namungo zimeshindwa kutambiana na kujikuta zikigawana pointi kwenye mchezo wa juzi uliochezwa Uwanja wa Mkwakwani, Tanga.

Jumatano iliyopita, Coastal ilipata ushindi wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu uwanja huo huo, ikiifunga Mashujaa FC mabao 2-0, huku Namungo nayo Ijumaa iliyopita ikapata ushindi wa kwanza ugenini, Uwanja wa Azam Complex wa mabao 3-1 dhidi wenyeji Azam FC, lakini juzi zilipokutana zimeshindwa kutambiana na kuendeleza mwendo wao wa kusuasua.

Timu zote mbili zilishinda mechi zake baada ya kuwaondoa makocha wao wakuu, Namungo ikiachana na Mrundi Cedric Kaze na Coastal ikimbadilishia majukumu kocha wake, Mkongomani Mwinyi Zahera ikimpa cheo cha Ukurugenzi wa Ufundi.

Timu hizo kwa sasa zinaongozwa na waliokuwa makocha wasaidizi, Fikirini Elias upande wa Coastal Union na Denis Kitambi kwa Namungo.

Katika mechi hiyo, timu zote zilionekana kushambuliana kwa zamu zikikosa mabao ya wazi, lakini hadi dakika 90 zinamalizika, hakuna iliyokwamisha mpira wavuni.

Matokeo hayo si mazuri kwa timu zote mbili kwani zimeendelea kukaa maeneo hatarishi kwenye msimamo wa ligi mpaka sasa, zote zikiwa na pointi saba.

Namungo ipo juu ya mwenzake, ikiwa nafasi ya 12, ikicheza mechi nane, ikishinda moja, sare nne huku ikipoteza mechi tatu, Coastal kwa upande wao wanakamata nafasi ya 13 ikiwa na pointi sawa na na Namungo, ikishinda mechi moja, sare nne na kupoteza michezo mtatu pia.

Mabao saba iliyofunga Namungo dhidi ya manne iliyofunga Coasta ndiyo yanayowatofautisha mmoja awe juu na mwingine chini.




Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Hamis Mwinjuma (katikati) na Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Dunstan Kyobya (wa pili kushoto) wakishuhudia Mkurugenzi wa Idara ya Fedha na Mwenyekiti wa klabu ya Gofu ya Kampuni ya Sukari Kilombero Fakihi Fadhili akikabidhi zawadi kwa mmoja wa washindi wa mashindano ya wazi ya mchezo huo ya Kilombero yaliyofanyika Oktoba 28-29 wilaya ya Kilombero. Wengine ni Mkurugenzi wa Biashara Kampuni ya Sukari Kilombero Fimbo Butallah (kulia) na Meneja wa Benki ya NMB tawi la Kilombero, Nelly Masisi.**PICHA:MPIGAPICHA WETU.**

# Pambano la Dula Mbabe, Katompa kutangaza utalii

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAKATI joto la pambano la ngumi kati ya bondia Abdallah Pazi 'Dula Mbabe' na Erick Katompa kutoka Congo likizidi kupanda, promota wa pambano hilo, Sophia Mwakagenda, amesema lengo la pambano hilo ni kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kutangaza utalii wa ndani.

Akizungumza na waandishi wa habari Jijini Dodoma katika viwanja vya Bunge, Mwakagenda alisema lengo la pambano hilo ni kutangaza utalii kama alivyofanya Rais Samia kupitia filamu ya Royal Tour, na pambano hilo litashuhudiwa na watu kutoka ndani na nje ya nchi.

Mwakagenda ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum, alisema wamepeleka pambano hilo katika Jiji la Arusha kwa sababu kipindi hicho ni msimu wa utulivu kwa watalii wanaotembelea Tanzania, hivyo miongoni mwa vitu watakavyopata ni burudani ya ngumi.

Alisema pambano hilo litafanyika Novemba 25 mwaka huu na linatajwa kuwa la kihistoria na kulipa kisasi.

"Pambano hilo litatanguliwa na mapambano mengine ya utangulizi tisa na watakaopanda ni wapiganaji wakali wakiwemo wanawake, kwa hiyo hakuna atakayejuta kufika kwenye uwanja wa vitasa, naomba watu wajitokeze," alisema Mwakagenda.

Kuhusu mshindi kupewa jina la mnyama, alisema mbali na zawadi nono ambayo mshindi ataibuka nayo, lakini atakuwa na nafasi ya kuchagua jina la mnyama anayemtaka na litalipiwa kwa niaba yake kama alama ya utambulisho kwa nchi.

Mwakagenda alisema kuwa mabondia kabla na baada ya mapambano yao watapata nafasi ya kutembelea mbuga za wanyama kuangalia vivutio ili wawe sehemu ya kuutangaza utalii wa nchi.

## Kocha Ihefu alia na mabeki wake

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Ihefu FC, Mosses Basena amesema katika michezo mitatu aliyoiongoza timu yake katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, amegundua kuwa kuna udhaifu mkubwa kwenye safu yake ya ulinzi.

Basena tangu amekabidhiwa kazi ya kukinoa kikosi cha timu hiyo imecheza michezo mitatu ikitoka sare mbili dhidi ya Coastal Union na Singida Fountain Gate FC na kupoteza mechi na Simba kwa mabao 2 -1.

Akizungumza na Nipashe jana, Basena alisema ameona mapungufu ya timu yake hasa safu ya ulinzi ambayo imekuwa imeruhusu mabao katika michezo miwili kati ya mitatu waliyocheza chini yake.

Alisema mechi yao dhidi ya Singida Fountain Gate FC walicheza vizuri safu ya ushambuliaji walitumia vizuri nafasi walizotengeneza lakini safu ya ulinzi imekuwa bado na changamoto.

"Changamoto kubwa iliyopo ni kushindwa kujipanga vizuri na kuokoa mipira ya kutengwa, kama kwenye mchezo na Singida Fountain Gate FC ambapo tuliwapa mwanya wa kufunga kirahisi, tunarudi uwanja wa mazoezi kufanyia kazi mapungufu haya," alisema Basena.

## Jux afunika uzinduzi simu

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa muziki wa kizazi kipya 'Bongofleva' Jux juzi alikonga mioyo ya mashabiki wake kwa burudani kali katika uzinduzi wa simu mpya.

Katika hafla hiyo, Jux pia alitangazwa kuwa balozi mpya wa simu aina ya OPPO.

Jux aliwanyanyua wafanyakazi wa kampuni hiyo na wageni waalikwa ambao waliimba na kucheza nyimbo mbalimbali za msanii huyo.

Akizungumza muda mfupi baada ya kushuka jukwaani Jux alisema ni fahari kwa wasanii wa kitanzania kupata nafasi kama hizo za ubalozi wa bidhaa kwani ni njia moja wapo ya kupata kipato na kujitangaza zaidi.

"Hii ni kampuni kutoka China lakini wameona umuhimu wa kuwekeza Tanzania kwa sababu ya mazingira bora yaliyowekwa na Serikali lakini pia wameona umuhimu wa kutumia wasanii wa ndani kutangaza bidhaa zao," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa OPPO Tanzania, Kenny Yue alitangaza rasmi kuingizwa katika soko laTanzania bidhaa zake nchini Tanzania zijulikanazo ka 'OPPO A series' na wanajivunia kuwapa ubalozi wasanii wa hapa nchini.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SUAREZ KUTUA INTER MIAMI

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Uruguay na Gremio, Luis Suarez mwenye umri wa miaka 36, anatazamiwa kujiunga na Inter Miami mwaka 2024 ambako ataungana na wachezaji wenzake wa zamani wa Barcelona kama vile Lionel Messi, Sergio Busquets na Jordi Alba. **(El Pais - kwa Kihispania)**

### TONEY AGOMBEWA ENGLAND

KLABU za Chelsea na Arsenal zinawania kumsajili Ivan Toney baada ya Brentford kuthibitisha kuwa watamuuza mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 27 kwa bei inayofaa. **(Express)**

### IVAN KUBAKIZWA

KLABU ya Brentford inamthaminisha Ivan Toney kuwa mwenye thamani ya pauni milioni 100 lakini wananuia kusalia naye hadi mwisho wa msimu. **(Sky Sports)**

### COSTA ANYATIWA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United inaendelea kutuma maskauti kumfuatilia mlinda mlango wa Ureno, Diogo Costa mwenye umri wa miaka 24 ambaye wamekuwa wakimnyatia kabla ya kumsajili mchezaji wa kimataifa wa Cameroon, Andre Onana. Lakini ataondoka Porto ikiwa United italipa euro milioni 75 za kifungu cha kutolewa. **(A Bola)**

### DAVIES AWINDWA

KLABU ya Real Madrid inamtaka mchezaji wa kimataifa wa Canada, Alphonso Davies mwenye umri wa miaka 22 na wana uhakika wa kukubaliana na klabu yake ya sasa ya Bayern Munich ili kumleta kwenye LaLiga msimu ujao. **(Relevo)**

### SESKO ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL inapanga kumnunua mshambuliajiwa Slovenia, Benjamin Sesko mwenye umri wa miaka 20, ambaye aliikataa Manchester United msimu uliopita na badala yake akajiunga na RB Leipzig. **(Mirror)**

### LUKAKU ASHUTUMIWA

MKURUGENZI wa michezo wa Inter Milan, Piero Ausilio amemshutumu mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku kwa utovu wa "nidhamu" kwa kuanzisha mazungumzo na Juventus huku majadiliano kati ya Chelsea na Inter yakiendelea na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 hatimaye kujiunga na Roma kwa mkopo. **(Mail)**

### EVERTON KUMPA MKATABA HARRISON

KLABU ya Everton iko tayari kumsajili winga wa Leeds United, Jack Harrison mwenye umri wa miaka 26 kwa mkataba wa kudumu. **(Teamtalk)**

### BOEY KWENYE RADA

KLABU ya Manchester United inavutiwa na beki wa Galatasaray na Ufaransa, Sacha Boey mwenye umri wa miaka 23, huku Arsenal, Brighton na Burnley pia zikimnyatia. **(Mail)**

### POTTER KUMRITHI TEN HAG

KOCHA wa zamani wa Brighton, Graham Potter huenda akawa kocha ajaye wa Manchester United baada ya tetesi kuashiria wanataka wamtimue Erik ten Hag. **(Mirror)**

### TCHOUAMENI HATARUHUSIWA

REAL Madrid 'hawana nia' ya kumruhusu kiungo wa Ufaransa, Aurelien Tchouameni kuondoka katika klabu hiyo huku Arsenal na Liverpool wakimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. **(90 Min)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CHELSEA, LIVERPOOL ZAKOMAA NA OSIMHEN

Yaelezwa ndio sababu mazungumzo ya nyota huyo na klabu yake ya Napoli kukwama...

**NAPLES, Italia**

MAZUNGUMZO ya mkataba mpya baina ya mshambuliaji, Victor Osimhen na Napoli yameripotiwa kusuasua na inadaiwa kuchangiwa na timu za Liverpool na Chelsea kumuhitaji staa huyo wa kimataifa wa Nigeria.

Osimhen ameanza msimu huu wa 2023-24 kwa kasi kubwa, akifunga mabao sita katika mechi nane za Serie A alizocheza hadi sasa, lakini amekuwa na shida nyingi za nje ya uwanja na klabu yake ya Napoli.

Mwezi uliopita, kambi ya Osimhen ilitishia kuiburuza mahakamani Napoli kutokana na kuposti video mbili za unyanyasaji kwa mshambuliaji huyo kwenye TikTok, ikiwamo moja ya kumdhihaki kwa kukosa penalti dhidi ya Bologna.

Napoli ilidai haikulenga kumuumiza Osimhen, huku jambo hilo likichochewa moto zaidi na uamuzi wa kocha Rudi Garcia kumtoa katika mechi dhidi ya Bologna.

Mapema mwezi huu, Rais wa Napoli, Aurelio de Laurentis alisema makubaliano ya awali ya mkataba mpya yalifikiwa kabla ya Osimhen kubadili mawazo ya kumwaga wino.

Kutokana na hilo, De Laurentis alisema anafikiria kumpiga bei Osimhen mwakani kabla ya kufikia mwaka wa mwisho wa mkataba wake baada ya kuona pande hizo mbili kutokuwa na uhusiano mzuri.

Osimhen inaaminika analipwa pauni milioni 3.9 kwa mwaka na anataka mshahara upande mara mbili ufike pauni milioni 78, lakini De Laurentiis hayupo tayari.

Mkataba wa Osimhen una kipengele kinachohitaji ilipwe pauni milioni 174.3 kwa timu itakayohitaji huduma yake.

Osimhen alitua Napoli kwa usajili ulioigharimu klabu hiyo pauni milioni 65.4 mwaka 2020.

HABARI MICHEZO



# REAL MADRID KUMSAJILI KEPA JUMLA

**MARID, Hispania**

KLABU ya Real Madrid ipo tayari kumsajili jumla golikipa, Kepa Arrizabalaga kutoka Chelsea, katika dirisha lijalo la majira ya joto lakini haipo tayari kulipa zaidi ya pauni milioni 17.5.

Mlinda lango huyo raia wa Hispania miaka mitano iliyopita alivunja rekodi ya kuwa kipa ghali zaidi duniani baada ya kusajiliwa akitokea Athletic Bilbao kwa pauni milioni 71.5 kwenda Chelsea.

Real Madrid imefikia uamuzi wa kumsajili Kepa kutokana na kiwango bora alichoonyesha baada ya kujiunga nayo kwa mkopo katika dirisha lililopita la majira ya joto.

Tangu msimu huu uanze Real Madrid imepoteza mechi moja ya LaLiga wakati Kepa akiwa golini.

Kepa alisajiliwa kwa ajili ya kuziba kwa muda pengo la Thibaut Courtois ambaye atakuwa nje kwa msimu mzima kutokana na majeraha ya goti yanayomsumbua.

Ili kufanikisha dili lake, Kepa anadaiwa kukubali hadi kupunguziwa mshahara wa pauni 175,000 kwa wiki anaoupokea ili kuiwezesha Madrid kumchukua.

Mkataba wake wa sasa na Chelsea unatarajiwa kumalizika 2025.

# Wachezaji Barca wamshangaza Gundogan

**BARCELONA, Hispania**

KIUNGO wa Barcelona, Ilkay Gundogan amefichua siri kwamba baadhi ya wachezaji wenzake hawakuumizwa na kichapo dhidi Real Madrid kwenye mechi ya El Classico uliochezwa Jumamosi.

Kiungo huyo alitamani kuona wenzake wakihuzunika katika vyumba vya kubadilishia nguo kufuatia kichapo cha mabao 2-1 ambayo yote yalifungwa na Jude Bellingham.

Gundogan ndiye aliyefunga bao la kuongoza kwa upande wa Barcelona kabla ya Bellingham kufunga mabao mawili na kuipa ushindi Madrid.

Kutokana na kichapo hicho Barcelona imeshuka mpaka nafasi ya tatu ikiwa nyuma kwa pointi nne dhidi ya Madrid na Girona kwenye msimamo wa LaLiga.

Gündogan alifichua siri kwamba: "Baada ya matokeo mabaya nilitarajia kuona hasira za wachezaji wenzangu ndani ya vyumba vya kubadilishia nguo.

"Ndio watu wamesikitika baada ya mechi hiyo kubwa, na matokeo kwa ujumla, nilitamani kuona hasira zaidi lakini hakuna kabisa. Unajua unaweza ukafanya vizuri katika mambo fulani lakini ukanyamaza." Alisema Gundogan.



Barcelona ilipoteza pointi tatu katika mechi tano za mwisho za LaLiga baada ya kutoka sare dhidi ya Mallorca na Granada.

Pia, ilianza msimu bila kufunga bao dhidi ya Getafe, na Gundogan amekiri kwamba timu inahitaji kuimarika zaidi.

"Tunatakiwa kupambana kwa sababu Real Madrid au Girona wana kasi, sikuja hapa kwa ajili ya kupoteza mechi dhidi ya timu kama hizi au kutengeneza uwiano kuwa mkubwa kwenye msimamo, aliongeza nyota huyo wa zamani wa Man City.

# Ni Mamelodi na Waydad fainali AFL

**CAIRO, Misri**

KLABU ya Mamelodi Sundowns ilitinga fainali ya Ligi ya Soka ya Afrika (African Football League) baada ya kutoka sare ya bila kufungana na Al Ahly Jumatano mjini Cairo, Misri.

Sare hiyo ilimaanisha kwamba, Mamelodi wamefuzu fainali baada ya mchezo wa kwanza kushinda 1-0 na sasa watacheza dhidi ya Wydad Casablanca.

Sare ya bila kufungana kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Cairo iliifanya Sundowns kusonga mbele baada ya ushindi wa mkondo wa kwanza wiki iliyopita.

Al Ahly walikuwa na presha kubwa tangu mwanzo huku Percy Tau akipata penalti ambayo iliokolewa na golikipa, Ronwen Williams.

Williams pia aliokoa hatari mbili za wazi kwa kuzuia juhudi za Al Ahly huku Sundowns wakinusurika na dhoruba ya mapema.

Sundowns ilitegemea ulinzi wa hali ya juu na bahati kuishinda timu ya Al Ahly iliyokuwa na nia ya kutwaa ubingwa huo.

Lakini Waafrika Kusini hao walionyesha ujasiri wa kukamilisha kazi katika usiku wa wasiwasi na kuandika jina lao kwenye michuano hiyo mipya ya AFL.

Ushindi huo wa mkondo wa kwanza ulionekana kuwa muhimu kwani Sundowns iliifungia Al Ahly kwa kuwapiga kaunta kupitia Thapelo Maseko Jumapili iliyopita.

Bao hilo la thamani la nyumbani hatimaye lilifanya tofauti juu ya michezo yote miwili huku Sundowns ikiendelea kushikilia ushindi huo maarufu wa jumla.

Sasa Mamelodi itacheza na Wydad ambayo iliitoa Esperance de Tunis kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 5-4.

Mshindi wa fainali hiyo ataibuka na kitita cha dola za Marekani milioni 4.



HABARI MICHEZO

# FEI TOTO ATAMBA AZAM IMEANZA LIGI

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa Azam FC , Feisal Salum 'Feitoto' amesema ushindi walioupata juzi wa mabao 3-0 dhidi ya Mashujaa FC umeinua morali yao na sasa wameanza rasmi Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza mara baada ya mechi hiyo ambayo Feitoto alitoa pasi mbili za mabao 'assist', alisema mashabiki wa timu hiyo watarajie muendelezo wa mambo mazuri kwa sababu wamekaa sawa na rasmi sasa wameianza ligi wakiwa ugenini, Uwanja wa Lake Tanganyika.

"Tulicheza kwa maelekezo ya mwalimu, kipindi cha kwanza wenzetu walikaa nyuma sana na mapumziko alituelekeza namna ya kucheza na kutegua mitego yao, ndiyo maana unaona tumepata mabao haya matatu, kusema kweli Mashujaa siyo timu mbaya, wana kikosi kizuri.

Nawaambia mashabiki wangu na wa Azam FC watarajie mazuri kutoka kwangu na kwa wachezaji wenzangu, sasa ndiyo tumeianza ligi," alisema Feitoto.

Aidha, Kocha wa timu hiyo, Bruno Ferry aliwashukuru wachezaji wake kwa kushinda mechi ngumu ugenini, huku akiwashukuru mashabiki wa Azam kwa kusafiri umbali mrefu kwenda kuwaunga mkono.

"Tulicheza tukiwa na presha ya kupoteza mechi mbili mfululizo dhidi ya Yanga na Namungo, lakini wachezaji wangu walitulia na kuwa imara, tumecheza na timu ngumu iliyo na mashabiki wengi wenye mzuka na mpira wa miguu," alisema Bruno.

Kwa upande wake, Kocha wa Mashujaa Mohamed Abdallah 'Bares', aliwaomba radhi mashabiki wa timu hiyo, akisema wamefedheeshwa na kipigo hicho.

"Tunaomba msamaha kwa mashabiki wote wa Kigoma, kusema kweli tumefedheeka, mipango yetu kwanza ili kuwa ni kuzuia kipindi cha kwanza, halafu tufunguke kipindi cha pili, kwa bahati mbaya sana tumefungwa mabao mepesi sana," alisema Bares.

Ni kipigo cha kwanza kwa Mashujaa kwenye uwanja wake wa nyumbani tangu kuanza kwa ligi na sasa imebaki na pointi nane, huku Azam ikikwea hadi nafasi ya tatu ikifikisha pointi 16 kwa mechi nane ilizocheza.




Msanii nyota wa Bongo fleva Jux (katikati) akijipiga selfie wakati wa uzinduzi wa simu mpya jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAHA yataka makocha kujinoa

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Chama cha mpira wa mikono Tanzania (TAHA) kimewasisitiza makocha kuendelea kuthibitisha ushiriki wa kozi ya ukocha leseni D ambayo itafanyika katika vituo viwili vya Mwanza na Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, Naibu Katibu Mkuu waTAHA, Yehoshefati Kalulu alisema kuwa milango ipo wazi na uthibitisho huo utaenda sanjari na ulipaji wa ada ya ushiriki ambayo ni kiasi cha shilingi 135,000.

Alisema ratiba ya kozi hiyo inaonyesha Mwanza itaanza Novemba 30 mpaka Desemba 6 mwaka huu, ikifuatiwa ile ya kituo cha Dar es Salaam itakayoanza Disemba 8 - 14 mwaka huu .

Alisema kuwa wale walioteuliwa na viongozi wa mikoa yao ili wapate fursa ya kushiriki kozi hiyo kwa manufaa yao binafsi, kimkoa pamoja na taifa kwa ujumla.

" Tayari tulitoa maelekezo kila mkoa uteuwe makocha ambao watahudhuria kozi hiyo kutoka Tanzania Bara na Zanzibar hilo limefanikiwa kwa asilimia 99 tunaomba kwa wale ambao hawajathibitisha wajitahidi ili wathibitishe," alisema Kalulu.

Alisema jumla ya washiriki 46 wa kozi hiyo wameteuliwa kutoka mikoa ya Zanzibar,Kigoma,Tabora,Rukwa,Kilimanjaro, Arusha,Tanga, Mbeya, Lindi ,Mtwara, Geita, Singida, Dar es Salaam, Pwani, Kagera, Ruvuma, Dodoma, Shinyanga na Morogoro.

Aliongieza kuwa mafunzo hayo yataendeshwa na Mkufunzi kutoka Shirikisho la Kimataifa la Mchezo huo (IHF), Klaus Feldmann.

# Simba yatamba kupiga kwenye mshono

INATOKA UK. 24

"Kwa majeruhi ni Aubin Kramo peke yake, yeye bado mwezi mmoja na nusu tu aweze kurejea dimbani, kikubwa tuko kamili kuelekea Jumapili," alitamba Ahmed.

Ahmed amewataka mashabiki kujitokeza kwa wingi kuangalia mechi hiyo inayozikutanisha timu pekee ambazo zinasaka ubingwa wa Tanzania Bara kwa vitendo.

"Hii ni mechi ambayo inabeba taswira ya mpira halisi wa Tanzania, hizi ndiyo timu mbili ambazo tangu ligi ianze unaona zinautaka ubingwa kwa vitendo na si kwa maneno kama zingine, lakini linapokuja mechi za dabi pia hazijawahi kuwa nyepesi hata moja wapo iwe mbovu kiasi gani, pamoja na kufungwa na Ihefu lakini Yanga ndiyo timu ngumu katika Ligi Kuu ya Tanzania Bara kwa sasa, hivyo tutaingia tukijua tunacheza na mpinzani ambaye tumemsoma vizuri ," alisema.

Mara ya mwisho timu hizo zilipokutana kwenye fainali ya Ngao ya Jamii, Agosti 13, Simba ilishinda kwa mikwaju ya penalti 3-1 , baada ya kutoka suluhu kwa dakika 90 za mchezo.

Msimu wa Ligi Kuu iliyopita 2022/23, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1, mechi ikichezwa Oktoba 23 mwaka jana na mzunguko wa pili, Simba iliifunga Yanga mabao 2-0 katika mechi iliyochezwa Aprili 16 mwaka huu.

# Gamondi: Nina dawa ya Simba

INATOKA UK. 24

fainali ya AFL ambapo alikuwa sehemu ya watazamaji kwenye Uwanja wa Mkapa katika mchezo huo uliomalizika kwa Simba kutoa sare ya mabao 2-2.

Mchezo mwingine ambao Gamondi aliushuhudia ulikuwa ule wa Ligi Kuu dhidi ya Ihefu ambao Simba waliibuka na ushindi wa mabao 2-1.

Kocha Gamondi atakuwa na kazi moja tu ya kuhakikisha anaipa ushindi timu yake ambayo kwenye mechi ya mwisho ya Ligi kuu dhidi ya Simba walipoteza kwa mabao 2-0.

# Michezo

Ijumaa Novemba 3, 2023

Nipashe




## Chelsea, Liverpool zakomaa na Osimhen

UKURASA 21



Wachezaji wa Azam FC, Kipre Junior na Charles Manyama wakimpongeza mshambuliaji Alassane Diao (aliyelala chini) baada ya kuifungia timu hiyo moja ya goli katika ushindi wa magoli 3-0 walioupata juzi usiku dhidi ya Mashujaa FC kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma. **PICHA: BINZUBERY**

# GAMONDI: NINA DAWA YA SIMBA

### ●●●Ni baada ya kuitazama kwa dakika 180, awaita mashabiki uwanjani jumapili...

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi amesema kwa muda alioitazama Simba kwenye michezo yake miwili ya hivi karibuni, anajua namna gani ya kupambana nao na kuhakikisha wanapata ushindi.

Kocha huyo raia wa Argentina amewataka mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi kuangalia mpira kwani anaamini utakuwa mchezo mzuri na wenye upinzani kutokana na aina ya vikosi vya timu hizo.

Gamondi, alisema amewatazama Simba na ameona ni timu nzuri yenye uimara na ubora na udhaifu kwenye baadhi ya maeneo na tayari wameshaanza kuyafanyia kazi madhaifu yao.

"Nimeiona Simba, ina ubora na udhaifu wake, pale kwenye udhaifu ndipo tunapotaka kuutumia ili tupate ushindi kwenye mchezo wetu wa Jumapili, mashabiki wana umuhimu mkubwa kwetu katika mchezo huo, tunawaomba waje kwa wingi" alisema kocha huyo.

Hata hivyo alisema hata timu yake nayo haijakamilika, na ina mapungufu ambayo hata hivyo ameendelea kuyafanyia kazi hasa idara yake ya ushambuliaji na mabeki.

"Nyuma tumekuwa na tatizo la kuruhusu mabao, lakini pia tumekuwa tukikosa sana mabao hasa washambuliaji, angalia mechi zetu nyingi zinaamuliwa na viungo, sehemu ambayo tuna ubora mkubwa kwa sasa," alisema kocha huyo.

Gamondi ametabiri kuwa itakuwa ni mechi nzuri na yenye mbinu kali kwa makocha na ufundi mwingi kwa wachezaji wa pande zote mbili.

"Itakuwa ni mechi nzuri ya mbinu na ufundi, tunajiandaa kwa ajili ya kutafuta ushindi na kujiweka katika nafasi nzuri katika mbio zetu za kutetea ubingwa wa ligi kuu," alisema Gamondi.

Yanga inajiandaa kukabiliana na Simba ikiwa tayari imekusanya pointi 18 baada ya kucheza mechi saba huku Simba pia wakiwa na pointi 18 baada ya kucheza michezo sita.

Gamondi alitumia dakika 90 za kwanza za mchezo wa robo

INAENDELEA UK. 23

# Simba yatamba kupiga kwenye mshono

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Simba umesema licha ya ukweli kuwa wapinzani wao Yanga wamebadilika kiuchezaji kulinganisha na msimu uliopita, hilo haliwatishi na halitawazuia kuibuka na ushindi kwenye mchezo huo wa Ligi kuu Tanzania Bara.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally alisema hayo jana alipokuwa akizungumzia mchezo huo unaosubiriwa kwa hamu na mashabiki na wapenzi wengi wa soka Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla.

Ahmed alisema wapinzani wao wanaonekana kuongezeka ubora msimu huu hasa kwenye kasi na kukaba.

"Zinapokwenda kucheza timu zinazoshika nafasi ya kwanza na nyingine ya pili, mechi hiyo haiwezi kuwa nyepesi, lakini pia tuseme ukweli mwalimu Gamondi ameibadilisha Yanga kutoka pale ambapo aliiacha kocha Nasreddine Nabi, kuna kitu amekiongeza, kwa hiyo mechi itakuwa ngumu," alisema Ahmed.

Hata hivyo alisema pamoja na yote hayo Simba ina kikosi cha wachezaji bora ambao wanaweza kuamua matokeo katika mechi yoyote ile.

"Simba tunayo faida ya kwenda kufanya vizuri dhidi yao kwa sababu tuna wachezaji bora zaidi yao, wachezaji wamecheza mechi nyingi kubwa na zenye presha, hatuna shaka hata kidogo, pamoja na uimara wao tutapiga pale pale tulipopiga kwenye mechi ya mwisho ya Ligi kuu tulipokutana msimu uliopita," alisema Ahmed.

Alisema wachezaji wao pamoja na kocha Roberto Oliviera 'Robertinho' wana uwezo mkubwa wa kuikabili Yanga na timu yoyote Afrika.

Alisema Robertinho anaendelea na maandalizi yake tangu Jumanne iliyopita kiufundi na kila kitu kinakwenda vizuri akiwa na wachezaji wake wote.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >